# *WIMBO ULIO BORA*: UFASIRI WA JAZANDA KWA MIKABALA
# KIDINI NA KIJAMII

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

NA

**KIROBI, J. T.**

**Tasnifu hii inawasilishwa kwa Shule ya Waliofuzu Kutimiza Baadhi ya M**
**ya Shahada ya Uzamili (M. A.) katika Kiswahili,**
**Chuo Kikuu cha Egerton.**

**Januari, 2006.**

## UNGAMO NA IDHINI

### UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijatolewa kwa mahitaji ya Shahada nyingine katika Chuo Kikuu chochote kile.

Kirobi, J.T. ---------------------------------- 25.03.2006 ----------------------

Sahihi Tarehe

### IDHINI

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu cha Egerton.

Dkt. Furaha Tchai ---------------------------------- 25 · 03 · 2006 ----------------------

Sahihi Tarehe

Dkt. James O. Ogola ---------------------------------- 25.3.2006 ----------------------

Sahihi Tarehe

## KUMBUKIZI

Kwa kumbukizi za Mwalimu mkuu wangu wa Sekondari, hayati Bw. William Gachanja Githinji. Alinitia shime na kuniadabisha katika masomo.

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa wapendwa wafuatao:

Bibi yangu Nduta Thuku,

Mtoto wetu Kirobi Thuku (Jomo),

wazazi wangu - Salome Wanjiru na

Mchungaji Peter Kirobi Mworia.

## SHUKRANI

Kazi ya utafiti si rahisi. Ni vigumu sana mtafiti kuifanya kwa ukamilifu peke yake. Basi, shukrani zangu za dhati ziwafikie wafuatao, waliotoa mchango wao kuuimarisha mradi huu. Kwanza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia heri na neema katika kipindi chote cha masomo yangu. Ninawashukuru sana wasimamizi wangu ambao pia ni wahadhiri wangu wa zamani Dkt. Furaha Tchai na Dkt. James O. Ogola. Mwongozo wao wenye uhakiki wa kina uliipa kazi hii mwelekeo bora. Aidha, walinisikiliza kwa makini kila nilipotoa hoja zangu japo wakati mwingine zikiwa dhaifu. Mungu awabariki sana. Dkt. S.Beja. Alinifunza Mbinu za Utafiti (kozi muhimu katika utafiti), na kila mara alizua maswali makali yenye kuchochea akili na kuijenga kazi hii. Bi. Rosemary Liguyani aliniauni pakubwa. Ninamshukuru mno kwa kuniazima tasnifu yake iliyonizindua. Nimeirejelea tasnifu hiyo katika kazi hii. Motisha niliopewa na wahadhiri wengine wa Idara ulinitia moyo sana. Hawa ni pamoja na Bw. G. Mayaka, Bw. W. Nabea na Bw. S. Gakero miongoni mwa wengine.

Babangu Mchungaji Peter Kirobi Mworia ninakushukuru kwa kuniazima miongozo ya Biblia.. Miongozo hiyo ilinisaidia sana na bila shaka nimeirejelea si haba tasnifuni. Ninamshukuru sana bibi yangu Nduta Thuku kwa kudhihirisha uwajibikaji nikiwa masomoni. Ninawashukuru wanafunzi wenzangu kwa mengi tuliyofanya pamoja. Mijadala na malumbano tuliyofanya kwa ushirikiano ilinijenga mno. Hawa ni Chomba Esther, Gacheiya Raphael, Muthigua Daniel na Ogola Roslyne. Bila woga, walinijulisha penye mushkili katika kazi yangu ambapo kwa hili, Raphael alikuwa msitari wa mbele. Kwa wanafunzi hawa ninashauri kwamba twendelee kushirikiana kama ndugu kwa kila hali; si katika masomo tu kwani chambilecho wahenga, umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Aidha, ninamshukuru Kimani, S.M. Tulijadili mengi pamoja yaliyonipa mwanga katika utafiti wangu. Ninaishukuru Tume ya Huduma kwa Walimu (T.S.C.) kwa kunipa likizo ya masomo yenye malipo. Ninawashukuru Peter na Jerusha wa P.K. Computers (Egerton) pamoja na Eli's Computer Center (Naivasha) kwa kuniruhusu nitumie tarakilishi zao. Walinisaidia kuinadhifisha tasnifu yangu. Ninamwombea dua Peter apate nafuu haraka ili awaauni wengine. Huenda kuna wengine wanaostahili shukrani zangu lakini nimesahau kuwataja kwa majina. Mungu anayewafahamu zaidi awakumbuke.

**IKISIRI**

Utafiti wetu ulihusu ufasiri wa jazanda zilizomo katika *Wimbo Ulio Bora*. Jambo hili linatokana na sababu kwamba usemi wa kidini, uwe zungumzwa au andikwa, haukosi kutumia jazanda miongoni mwa mbinu zingine. Pili, jazanda ni fumbo lenye maana fiche. Katika kufasiri jazanda moja, maana mbalimbali huzuka kutegemea tajriba, mitazamo ya kilimwengu, mahitaji na miktadha ya wale wanaohusika. Hali hii inaashiria kwamba, kama fumbo linalohitaji kufumbuliwa, jazanda huzua utata wa kifasiri kama ilivyodhihirika katika *Wimbo Ulio Bora*. Aidha, ni mchango katika fasiri chache zilizoko za *Wimbo Ulio Bora* na hivyo kuwa muhimu kwa wasomi na wahakiki wa Biblia. Bila shaka, tasnifu hii imeongeza ujuzi katika nyanda za usemi na uchanganuzi wa matini. Katika tasnifu hii, maana mbalimbali za jazanda za *Wimbo Ulio Bora* zilifafanuliwa, kwa mikabala ya kidini na kijamii na pia ikadhihirishwa jinsi jazanda za kidini za wimbo huu zinavyoweza kutumika katika miktadha ya kijamii. Utafiti ulikuwa wa kipekuzi. Data ilikusanywa kwa kusoma na kupekua yaliyomo katika Biblia lakini kwa wingi *Wimbo Ulio Bora* na miongozo mbalimbali ya Biblia. Uchanganuzi ulifanywa kwa njia ya maelezo. Matokeo ya muradi huu ni kwamba maana mbalimbali za jazanda za *Wimbo Ulio Bora* zimefafanuliwa kwa mikabala ya kidini na kijamii. Pia jazanda zake, licha ya kuwa semi za kidini, ilidhihirika jinsi zinavyoweza kutumiwa hata katika miktadha anuwai ya kijamii. Kwa kuzingatia matokeo ya tasnifu hii, tumehitimisha kwamba, jazanda ni fumbo na ufasiri wake hutegemea pakubwa miktadha na haja za wanajamii. Kufasiri jazanda za *Wimbo Ulio Bora* kwa mkabala mmoja tu (wa kidini), ni kufinya upeo wa matumizi yake.

# ABSTRACT

Our research involved interpretation of metaphors found in the *Song of Songs*. This issue emerges from the fact that religious discourses, whether oral or written, mostly employ metaphors among other stylistic features. Secondly, metaphors have hidden meanings. While interpreting a metaphor, a multiplicity of meanings emerges depending on experience, worldviews, needs and contexts of the persons concerned. This condition implies that, metaphors create ambiguity of interpretation as evidenced in the *Song of Songs*. This research is a contribution to the few existing interpretations of this song and hence becomes important to Bible readers and interpreters. It has also contributed to areas of discourse and textual analysis. Through this study, varied metaphorical meanings from the *Song of Songs* were established on religious and literal perspectives and it was also proved how these religious metaphors could be used in implied social contexts. This was content - analysis research. Therefore, data was collected through reading and analysing Biblical content with a bias to the *Song of Songs* and different Bible commentaries. The data was analysed descriptively. The result of this study is that different metaphorical meanings from this song have been established through religious and literal perspectives. Also, despite being religious, it was revealed how these metaphors can be used in a variety of implied social contexts. Considering the nature of the results, the study has concluded that the interpretation of any metaphor greatly depends on contexts and needs of individual participants. To interpret the metaphors of this song on one perspective only (religious) is to lessen their uses.

## FAHARASA

UNGAMO NA IDHINI ..... II

KUMBUKIZI ..... III

TABARUKU ..... IV

SHUKRANI ..... V

IKISIRI ..... VI

ABSTRACT ..... VII

FAHARASA ..... VIII

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ..... 1

1.1 Utangulizi ..... 1

1.2 Usuli wa Mada ..... 1

1.3 Mada ya Utafiti ..... 2

1.4 Madhumuni ya Utafiti ..... 2

1.5 Nadharia Tete za Utafiti ..... 2

1.6 Umuhimu wa Utafiti ..... 2

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti ..... 3

1.8 Ufasili wa Istilahi ..... 3

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI ..... 4

2.1 Utangulizi ..... 4

2.1.1 Anwani ya *Wimbo Ulio Bora* ..... 4

2.1.2 Maana ya Jazanda ..... 5

2.1.3 Jazanda na Ufasiri ..... 7

2.2 Misingi ya Nadharia ..... 14

2.2.1 Uainishaji wa Leech ..... 15

2.2.2 Pragmatiki ya Grice ..... 16

2.2.3 Ethnografia ya Mawasiliano ..... 18

SURA YA TATU: NJIA ZA UTAFITI ..... 20

3.1 Utangulizi ..... 20

3.2 Historia ya Chimbuko la *Wimbo Ulio Bora* ..... 20

3.3 Uteuzi wa Sampuli ..... 22

3.4 Ukusanyaji wa Data ..... 23

3.5 Uchanganuzi wa Data ..... 24

3.6 Hatua za Kuchanganulia Jazanda kutokana na Misingi ya Nadharia ........................ 26

SURA YA NNE: MATOKEO YA UTAFITI ........................ 30

4.1 Utangulizi ........................ 30

4.2 Muktadha ambamo Wimbo Uliimbwa ........................ 30

4.3 Mkabala wa Kidini wa Jazanda za *Wimbo Ulio Bora* ........................ 31

4.4 Hitimisho la *Wimbo Ulio Bora* kwa Mkabala wa Kidini ........................ 50

4.5 Mkabala wa Kijamii wa Jazanda za *Wimbo Ulio Bora* ........................ 51

4.6 Jazanda za *Wimbo Ulio Bora* na Miktadha ya Kijamii ........................ 56

4.6.1 Utongozaji ........................ 56

4.6.2 Uchumba ........................ 59

4.6.3 Ndoa ........................ 62

4.7 Hitimisho la jazanda za *Wimbo Ulio Bora* na Miktadha ya Kijamii ........................ 65

SURA YA TANO: MUHTASARI,HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................ 66

5.1 Utangulizi ........................ 66

5.2 Muhtasari wa Matokeo Makuu ........................ 66

5.3 Hitimisho ........................ 67

5.4 Mapendekezo ........................ 68

5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi ........................ 69

MAREJELEO ........................ 70

KIAMBATISHO ........................ 72

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Utangulizi

Sura hii ndiyo utangulizi wa muradi wetu wa utafiti. Katika sehemu ya kwanza, mambo muhimu kuhusu usuli wa mada yameelezwa kwa kifupi. Sehemu ya pili ni mada ya utafiti ambapo tatizo linaloshughulikiwa na utafiti huu limebainishwa. Madhumuni ya utafiti huu yameainishwa katika sehemu ya tatu ilhali nadharia tete za utafiti zimetajwa katika sehemu ya nne. Sehemu ya tano inaeleza umuhimu wa utafiti huu. Katika sehemu ya sita, upeo na mipaka ya kazi hii imebainishwa huku istilahi tata zikifasiliwa katika sehemu ya mwisho.

### 1.2 Usuli wa Mada

Jamii hujengwa kwa mihimili mingi, lugha ikiwemo. Lugha huwa andikwa au zungumzwa. Kwa vyovyote vile, lugha ni chombo cha mawasiliano. Dini ni asasi iliyoenziwa sana katika jamii hasa kwa kukuza maadili. Asasi hii hutumia lugha kupitisha ujumbe kwa wafuasi wake. Sawyer katika Mesthrie (2001:262) anadokeza kwamba, dini imechangia pakubwa katika historia ya lugha na isimu. Anaendelea kusema kuwa matini za kidini zina jukumu muhimu katika tamaduni za kidini na kwa hivyo lugha ambayo kwayo dini hiyo huandikwa na kusomwa ni muhimu. Dini ya Kikristo hutegemea sana Biblia katika kuendeleza mafunzo yake. Waandishi wengi wa Biblia walitumia jazanda katika sehemu nyingi walizoandika. Lakoff na Johnson (1980:3), wanasema kwamba jazanda hujikita katika maisha ya kila siku, sio tu katika lugha bali katika fikra na vitendo. Matumizi ya jazanda hufanya matini za Biblia kupewa fasiri mbalimbali na wasomi wake. Hali hii hutokana na utata ulioko katika kuzifasiri jazanda hizo. Kuhusiana na matini za kidini, Goldingay (1995:55), asisitiza kwamba wahubiri hamsini wanaweza kuzua mitazamo tofauti kutoka kwa matini moja. Goldingay anaongeza kwamba, maana ya matini ya Biblia hupatikana kutoka kwa hadhira na matini moja inaweza kueleweka kwa njia tofauti na wasomaji tofauti tofauti, Goldingay (1995:40). Kama kipengele cha matumizi ya lugha, jazanda hupewa maana na wasomaji wa Biblia.

Kutokana na kauli hii, mtafiti alizifafanua jazanda mbalimbali za *Wimbo Ulio Bora* kwa mikabala ya kidini na kijamii. Aidha, mtafiti alidhihirisha jinsi jazanda za kidini za wimbo huu zinavyoweza kutumika katika miktadha ya kijamii.

### 1.3 Mada ya Utafiti

*Wimbo Ulio Bora* ni mojawapo ya vitabu vya Biblia ambavyo vimekumbwa na utata wa kifasiri. Katika Wimbo huu, utata unachochewa zaidi na matumizi ya ushairi ambao umebeba jazanda nyingi. Aidha, haibainiki wazi wimbo huu ulitazamiwa kufasiriwa kwa mkabala upi. Tumefafanua jazanda zilizomo katika wimbo huu kwa mikabala ya kidini na kijamii.

### 1.4 Madhumuni ya Utafiti

i) Kufafanua maana mbalimbali za jazanda za *Wimbo Ulio Bora* kwa mikabala ya kidini na kijamii.

ii) Kudhihirisha jinsi jazanda za *Wimbo Ulio Bora* zinavyoweza kutumika katika miktadha ya kijamii.

### 1.5 Nadharia Tete za Utafiti

i) Jazanda za *Wimbo Ulio Bora* zinaweza kufafanuliwa kwa mikabala ya kidini na kijamii.

ii) Inawezekana kudhihirisha jinsi jazanda za *Wimbo Ulio Bora* zinavyoweza kutumika katika miktadha ya kijamii.

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa kazi hii ni pamoja na:

a) Kutoa mchango katika fasiri chache zilizomo za *Wimbo Ulio Bora.*

b) Kuupa *Wimbo Ulio Bora* mkabala mpya wa kifasiri; mkabala wa kijamii.

c) Kutatua utata uliomo wa kufasiri jazanda zilizomo katika *Wimbo Ulio Bora* kwa kuweka mpaka kati ya mkabala wa kidini na ule wa kijamii.

d) Kukuza na kuendeleza misingi ya nadharia iliyouongoza utafiti huu.

e) Kuzua mwongozo wa kufasiria jazanda zilizomo katika *Wimbo Ulio Bora*.

f) Kudhihirisha kuwepo kwa maingiliano kati ya dini ya Kikristo na maswala ya kijamii.

## 1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Kwa jumla, kitabu kimoja kilishughulikiwa ambacho ni *Wimbo Ulio Bora*. Jazanda zilizomo katika kitabu hiki zilifasiriwa. Vilevile, tuligundua kwamba wimbo huu umetumia mbinu nyingine za lugha kama vile tashbihi, chuku na taharuki. Hata hivyo, utafiti wetu ulijihusisha na ufasiri wa jazanda peke yake kwa mikabala ya kidini na kijamii. Pia, matumizi ya jazanda za *Wimbo Ulio Bora* katika miktadha ya kijamii yalidhihirishwa. Kwa vile utafiti huu ulikuwa wa upekuzi wa yaliyomo katika Wimbo Ulio Bora, nakala za matoleo mbalimbali za Biblia pamoja na nakala za miongozo mbalimbali ya Biblia zilikuwa marejeleo muhimu ambayo yalitegemewa sana katika kazi hii

## 1.8 Ufasili wa Istilahi

Ufasiri - Ufafanuzi wa maana katika neno au sentensi.

Jazanda - Mbinu ya lugha ambayo hulinganisha vitu ama watu bila kutumia viunganishi: kama, mfano wa, mithili ya, na sawa na.

Muktadha - Hurejelea washiriki, mahali na kitendo kinachohusika.

Mkabala - Ni mtazamo au Jinsi ya kuangalia jambo.

Ufasiri kwa mkabala wa kidini - Kuzifafanua jazanda kwa mtazamo wa kidini.

Ufasiri kwa mkabala wa kijamii - Kuzifafanua jazanda kwa mtazamo wa kijamii.

Kizungumzwa - Kitu kinachorejelewa katika jazanda.

Kifananishi - Kitu kinachoshabihishwa kwa kingine katika jazanda.

Kiungo - Sifa iliyo sawa kati ya kizungumzwa na kifananishi.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tunatalii yale yaliyoandikwa kuhusiana na mada yetu ya utafiti. Tumefanya hivyo kupitia kwa sehemu tatu kuu. Katika sehemu ya kwanza, (Anwani ya *Wimbo Ulio Bora*), tunatoa ufafanuzi wa anwani ya kitabu cha *Wimbo Ulio Bora*. Katika sehemu ya pili (Jazanda na ufasiri), tunatoa fasili ya jazanda huku tukihakiki maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu dhana hii. Aidha, tunaeleza jinsi ya kufasiri jazanda huku tukilinganisha maoni mbalimbali ya wasomi waliotangulia. Katika sehemu ya tatu (Misingi ya Nadharia), tunafafanua misingi ya nadharia ambazo zinaongoza utafiti huu. Tunaeleza nguzo za kila nadharia na jinsi nguzo hizo zinavyotuongoza katika uchanganuzi wa Data yetu.

### 2.1.1 Anwani ya *Wimbo Ulio Bora*

Katika Biblia, *Wimbo Ulio Bora* ni kitabu cha 22 kati ya vitabu 39 vya Agano la Kale. Wimbo huu uliandikwa na mfalme Sulemani. Barker (1995:997), akifafanua anwani *Wimbo Ulio Bora,* anasema kuwa anwani hii katika matini ya Kiebrania ni *Wimbo wa Sulemani* kumaanisha aidha wimbo ulioandikwa na Sulemani, au Wimbo wa Sulemani au wimbo kumhusu Sulemani. Anwani *Wimbo Ulio Bora* inamaanisha wimbo ulio mkuu miongoni mwa nyimbo nyingine kama ilivyo katika Kumbukumbu la Torati 10:17, "Mungu wa miungu" na "Bwana wa mabwana" na katika Timotheo wa Kwanza 6:15, "Mfalme wa wafalme".

Sulemani alikuwa na wasifu wa utunzi wa nyimbo. Kulingana na kitabu cha Wafalme wa Kwanza 4:32, Sulemani alitunga jumla ya nyimbo 1005. Wimbo huu ndio uliokuwa maarufu sana na ndio sababu ukatajwa kuwa mkuu kuliko nyingine.

Barker anaendelea kusema kuwa wimbo huu unaashiria upendo kati ya Mungu na Israeli au kati ya Mungu na kanisa. Wimbo huu unaoana na sanaa nyingi za kimapenzi za tamaduni mbalimbali kwa kutumia jazanda, zenye kuibua hisia kwa hali ya juu, zilizochotwa kutoka kwa mazingira.

Irwin (1986:228) anatoa kauli kwamba fasiri za *Wimbo Ulio Bora* ni nyingi na zenye utofauti. Kulingana na Irwin, fasiri sahili kabisa na halisi zaidi huonekana kama ni ile inayouchukulia kama ushairi au "drama" ya ndoa changa. Scofield (1992), akimuunga mkono Irwin, anaainisha ufasiri wa wimbo huu kwa njia tatu kama ifuatavyo:

1. Mapenzi ya Sulemani kwa msichana wa Shulama.
2. Upendo wa Mungu kwa watu wa Israeli.
3. Upendo wa Kristo kwa kanisa.

Baxter (1973:171) anaendeleza hoja kwamba wimbo huu ni zaidi ya wimbo wa mapenzi kati ya wapendanao. Kuna maudhui yenye mtazamo wa kidini. Hata hivyo, anatoa rai kuwa hakuna kitabu cha Biblia ambacho kimewahi kuandikiwa miongozo mingi yenye utofauti wa maoni kama ushairi huu mfupi wa beti nane. Ni wazi kwamba, maoni haya "anuwai yenye utofauti" yanadokeza kwamba kuna utata mkuu katika ufasiri wa wimbo huu.

### 2.1.2 Maana ya Jazanda

Katika kuzungumza na kuandika, mbinu anuwai za lugha hutumiwa. Jazanda ni mojawapo kati ya mbinu hizo. Jazanda ni mbinu ambayo hulinganisha vitu na vitu vingine, watu na vitu, watu na watu wengine au watu na viumbe. Huu ni ulinganisho usio wa moja kwa moja ambao kwao, kitu kimoja huitwa kingine bila kutumia viunganishi linganishi vifuatavyo:

- Mithili ya
- Mfano wa
- Sawa na
- Kama

Kwa mujibu wa Wallah (2000:xxv), jazanda ni mfano, picha au taswira ya kufananisha kiumbe chochote au kitu na binadamu kwa kukipa sifa au nafasi ya kibinadamu. Pia ni kumfananisha binadamu na kiumbe ama kitu kingine kwa kumwita jina la kitu hicho kwa maana ya kuwa sifa zao ni moja. Kutokana na kijelezi hiki cha Wallah (2000), swala muhimu la ufanano linajitokeza. Kitu kimoja kitaitwa kwa jina la kitu kingine iwapo sifa zao mahsusi zinafanana; la sivyo, ulinganishaji huo hautakuwa na msingi maridhawa.

Kando na jazanda, kuna mbinu ya tashbihi. Tashbihi imekaribia sana jazanda katika ulinganishaji ila tu kwamba tashbihi ni ulinganishi wa moja kwa moja wa vitu viwili au zaidi vilivyo na sifa sawa kwa kutumia maneno ya viunganishi linganishi. Kuhusiana na mfanano na utofauti kati ya mbinu hizi mbili, Syambo na Mazrui (1992:xv) wanasema kuwa mbinu ya jazanda inafanana sana na ile ya tashbihi kwa vile zote zinashabihisha sifa ya kitu kimoja na kingine. Tofauti iliyoko ni kwamba katika tashbihi, yale mambo mawili yanayoshabihishwa hutokezwa wazi wazi, moja likawekwa kando ya mwenziwe, pindi katika jazanda mambo yenyewe huunganishwa yakawa dhana moja. Mifano ifuatayo inaweka wazi tofauti hii:

Tashbihi:

(1a): Giza lilitufunika kama blanketi.

(2a): Sauti zilijitokeza kila upande zikapaa kama ving'ora.

(3a): Idi ameoa mke mkali mfano wa chui.

(4a): Gari la Obadia linaenda polepole mithili ya konokono.

(5a): Olerana amekuwa mzito kama nanga siku hizi.

Jazanda:

(1b): Blanketi la giza lilitufunika.

(2b): Ving'ora vya sauti vilijitokeza kila upande.

(3b): Idi ameoa chui.

(4b): Gari la Obadia limekuwa konokono.

(5b): Olerana amekuwa nanga siku hizi.

Kwa hivyo, jazanda ni fumbo lililofumbwa zaidi kuliko tashbihi; maana yake ni fiche mno kuliko ile ya tashbihi. Iwapo ni msisitizo, jazanda husisitiza jambo fulani zaidi kuliko tashbihi. Tumegundua kwamba jazanda hutumiwa na waandishi au wazungumzaji kwa sababu tofauti tofauti kama vile:

- Kusisitiza.
- Kulinganisha.
- Kusifu.
- Kukashifu
- Kuonyesha umahiri katika lugha husika.

Matumizi ya viunganishi kama inavyobainika katika mifano ya tashbihi (1a-5a), ndicho kigezo tulichokitumia kutambulisha jazanda katika *Wimbo Ulio Bora.* Kwa hivyo, tulijikita katika linganishi ambazo hazijatumia maneno ya kulinganisha. Tashbihi hutumia maneno ya kulinganisha ilhali jazanda haziyatumii ila kitu kimoja huitwa kingine.

### 2.1.3 Jazanda na Ufasiri

Dhana ya jazanda imejadiliwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwao ni Leech (1969), Mulokozi na Kahigi (1979), Lakoff (1980), Davidson (1984), Imbosa (1990), Davis (1991), Syambo na Mazrui (1992), miongoni mwa wengine. Kulingana na Lakoff na Johnson (1980:1), jazanda, kwa watu wengi ni mbinu ya kishairi yaani matumizi ya lugha ya kifasihi. Kinyume chake ni kwamba, jazanda ni zaidi ya hivyo kwani jazanda hutumika kila siku na katika miktadha mingi; sio tu katika lugha lakini katika mawazo na vitendo. Ili kuonyesha maana ya jazanda kuwa huunda tukio la kila siku, hebu tuangalie mfano wa dhana ya ubishi (argument) na jazanda iliyodhanaishwa ya ubishi ni vita (argument is war). Jazanda hii huakisiwa katika sura mbalimbali za lugha ya kila siku.

(6): Ubishi ni vita:

Madai yako hayakingiki.
Alishambulia kila hoja dhaifu katika maoni yangu.
Uhakiki wake ulilenga shabaha.
Niliangamiza maoni yake.
Sijawahi kumshinda katika mjadala.
Hukubali? Sawa, vurumisha!
Ukitumia mkakati huo, atakumaliza kabisa.
Alitungua maoni yangu yote.
Lakoff na Johnson (1980:4)

Ni muhimu kuona kwamba hatuzungumzi tu kuhusu mabishano kwa mkabala wa vita. Kwa kweli, tunanaweza kushinda au kushindwa katika mabishano. Tunaona mtu tunayebishana naye kama mpinzani. Tunamshambulia huku tukijikinga. Tunamiliki na kushindwa katika mabishano. Tunapanga na kutumia mikakati mipya.

Mambo mengi tufanyayo na kusema katika mabishano yanachukua muundo wa dhana ya kivita.

Japokuwa hakuna tukio halisi la kivita, kuna vita vya maneno, na muundo wa ubishi-ushambuliaji, ukingaji na kadhalika hudhihirisha hayo. Sio kwamba ubishi ni kipengele cha kivita, la hasha! Ubishi na vita ni vitu viwili tofauti. Hata hivyo, ubishi unaundwa kwa upande mmoja, kueleweka, kuendeshwa na kurejelewa kwa mkabala wa kivita. Dhana ya ubishi imechukua muundo wa kijazanda, tukio limeundwa kijazanda na hatimaye lugha imeundwa kijazanda. Kwa hivyo, msingi wa jazanda ni kuelewa na kuona kitu kimoja kwa msingi wa kitu kingine. Lakoff na Johnson (1980:5)

Jazanda hurejelea vidokezi vya maana ambavyo yawezekana vimelengwa na mzugumzi. Searle katika Martinich (1990:409), amebaini maana mbili za jazanda; maana ya usemi wa mzungumzi na maana ya neno au sentensi. Aghalabu, maana ya kijazanda ni maana ya usemi wa mzungumzi. Kwa kumrejelea Johnson katika Martinich (1990:409), Searle ameongezea kwamba jazanda huzua fikra mbili kwa pamoja. Kwa maoni yetu, fikra hizi mbili ni zile dhana za maana ya juu na maana ya ndani katika jazanda iwayo ile.

Syambo na Mazrui (1992:xv) wanasema kuwa mbinu ya jazanda inafanana sana na ile ya tashbihi, kwani zote zinashabihisha sifa ya kitu kimoja na kingine. Tofauti iliyoko ni kwamba katika tashbihi, yale mambo mawili yanayoshabihishwa hutokezwa waziwazi, moja likawekwa kando ya mwenziwe, pindi katika jazanda mambo yenyewe huunganishwa yakawa dhana moja.

(7): Katika tashbihi tutasema kuwa giza lilitufunika kama blanketi au sauti zilijitokeza kila upande zikapaa kama ving'ora. Katika jazanda tutasema kuwa blanketi la giza lilitufunika na ving'ora vya sauti vilijitokeza kila upande. Syambo na Mazrui (1992:xv).

Nasiri (1980:16) ametumia jazanda katika *Inkishafi.* Kwa mfano anafananisha dunia na bahari anaposema katika ubeti wa 13 kwamba:

8): Suu ulimwengu bahari tesi
        una matumbawe na mangi masi
    Aurakibuo juwa ni mwasi
        Kwa kulla khasara ukhasiriye

Dunia ni kama bahari iliyochafuka; yenye mawimbi makali na mawe makubwa ndani ya bahari (matumbawe) yanayoweza kuangamiza waliomo mle. Hili ni onyo kwa walimwengu wajihadhari na ulimwengu uliojaa maovu (masi). Pia amemithilisha dunia na mzoga katika ubeti wa 19 anaposema kuwa:

(9): Dunia ni jifa siikaribu
        Haipendi mtu ila kilabu
    I hali gani, ewe, labibu
        Kuwania na mbwa hutukizwaye?

Katika hali halisi, dunia haiwezi kuwa bahari tesi wala tulivu. Vilevile, dunia haiwi mzoga. Alichofanya mtunzi ni kuchukua sifa za bahari inayokabiliwa na mchafuko na kuzihamisha kwa dunia ambayo inanaweza kumwangamiza mtu asiyethamini uadilifu. Kwa njia hiyo, Nasiri amefananisha ulimwengu na mzoga wenye kutoa harufu ya kuudhi na hali hii haimaanishi kuwa dunia ni mzoga wala mzoga hauwi dunia. Maana ya mtunzi tutaitambua kwa kurejelea nia yake ya kusema maneno yale. Nia yake hasa ilikuwa kuusihi moyo wake ujiepushe na hadaa za ulimwengu na badala yake umwabudu Mwenyezi Mungu.

Walibora (1996:1) ametumia jazanda pale anapomfananisha babu yake Kongowea Mswahili anayeitwa mzee Mwinyi Makame na mti mkuu. Pia anaifananisha aila ya mzee huyo na ndege kwa maneno haya:

(10): Mti mkuu ukianguka, ndege huwa mashakani.

Mwinyi Makame hawezi kuwa mti wala aila yake (wake na watoto) hawawezi kuwa ndege. Anachofanya Walibora ni kufananisha mzee Mwinyi na mti mkuu (mti ulioishi miaka mingi) ilhali familia yake inafananishwa na ndege ambao huufanya maskani yao. Ufananishaji wa aina hii ndio uliotuongoza katika kutambulisha na kuchanganua jazanda za *Wimbo Ulio Bora*.

Davidson (1984:249) anasema kuwa jazanda ni kazi ya kinjozi ya lugha na, kama kazi zote za kinjozi, ufasiri wake hudhihirika kwa mfasiri kama katika asili yake (mnenaji). Ufasiri wa njozi huhitaji ushirikiano kati ya mwotaji na mfasiri; na kitendo cha ufasiri wa ndoto ni kazi ya ubunifu.
Vivyo hivyo, uelewaji wa jazanda ni jaribio la ubunifu kama ilivyo na uundaji wa jazanda. Anaendelea kusema kuwa jazanda humaanisha vile maneno, katika ufasiri wake wa kijuu juu humaanisha wala si zaidi. Jazanda ni aina ya utata kwani katika muktadha wake, maneno fulani yana aidha maana mpya au maana asili.

Msukumo wa jazanda hutegemea kukosa uhakika kwa upande wa msomaji au msikilizaji hali ambayo humfanya ayumbeyumbe kati ya maana mbili. Kuambatana na jambo hili, hebu tuangalie mfano ufuatao uliotolewa na Melville katika Davidson (1984:249).

(11): Kristo alikuwa kronometa (kipimawakati).
Katika mfano huu, athari ya jazanda inazuka kwa sababu yetu kuchukua kronometa kwanza katika maana yake halisi na baadaye katika hali isiyo ya kawaida. Katika matumizi ya jazanda kwenye *Wimbo Ulio Bora*, hali si tofauti na hii iliyoelezewa na Melville kwani jazanda hizo hukanganya na mwishowe huishia kupewa maana zenye utofauti na wasomaji tofauti tofauti wa wimbo huu. Sifa hii ya jazanda kuweza kukanganya iliwafanya Barfield na Black katika Davidson (1984:262) kusema kuwa, "aghalabu jazanda zote huongea uongo kwani jazanda husema jambo moja na humaanisha lingine". Naye Davis (1991:489) anasema kuwa jazanda huashiria vitu vingi kwetu kwa wakati mmoja. Hii ni hali ya utata. Bergmann katika Davis (1991:490) anabainisha sifa za jazanda kama ifuatavyo:

1. Jazanda huwa na uwazi kuliko tamathali zingine za lugha. Kwa mfano kinaya huashiria maana kwa njia ya kinyume. Kinachomaanishwa huwa ni kinyume cha kinachoashiriwa. Kwa upande mwingine uhusiano katika chuku ni wa kuongeza chumvi.
2. Kuelewa jazanda huhitaji zaidi ya kuelewa maana ya maneno.
3. Jazanda inapotumika kusisitiza jambo, haiwezekani kutolewa kauli iliyorahisishwa.
-. Hakuna sababu moja mahsusi ya kutumia jazanda.

Kwa maoni yetu, tungependa kubainisha maoni haya ya nne ya Bergmann katika Davis (1991:490) kwa kusema kuwa jazanda inaweza kutumiwa kwa sababu nyingi kama vile kusisitiza, kulinganisha, kusifu, kukashifu au hata kama njia ya kisanaa ya kujieleza kuonyesha umahiri katika lugha husika

Maelezo haya yanatuelekeza katika ukweli kuwa maana ya jazanda haiwezi kueleweka bila kuelewa maana ya kijuu juu. Vilevile, sifa za vitu vinavyofananishwa sharti zifahamike ili mlingano ule ukaribiane. Ujuzi huu ndio uliotuongoza katika kazi hii kupata fasiri zinazoafiki miktadha mbalimbali ya kidini na kijamii.

Goldingay (1995:55) asisitiza ukweli kwamba wahubiri hamsini wanaweza kuzua mitazamo tofauti kutoka kwa matini moja. Pia, maana ya matini ya Biblia hupatikana kutoka kwa hadhira na matini moja inanaweza kueleweka kwa njia tofauti tofauti na wasomaji tofauti. Kwa maoni yetu, sababu moja ambayo inanaweza kusababisha matini moja ya Biblia kupewa maana tofauti na wasomaji au wasikilizaji tofauti tofauti, ni matumizi ya jazanda ambazo kila msomaji au msikilizaji hufasiri kulingana na tajriba yake ya awali au mahitaji yake binafsi.

Kuhusu ufasiri, Brown (1995:25) anapendekeza kwamba, ni muhimu swala la ufasiri linapofikiriwa, nia ya msikilizaji katika kusikiliza ifikiriwe. Brown anaelekea kusema kuwa, msikilizaji au msomaji husikiliza au husoma matini akiwa na nia fulani. Muktadha ambamo hadhira hujikuta kwayo huweza kudhihirisha nia zao katika kusikiliza au kusoma matini andishi. Msingi mmoja wa nadharia uliotuongoza katika kazi hii (Ethnografia ya Mawasiliano), unathibitisha madai haya hususan kitengo chake cha tatu ambacho ni lengo/malengo – (rejelea sehemu ya 2.2.3) kwa maelezo zaidi. Katika muktadha wa utafiti huu, nafasi ya hadhira inachukuliwa na msomaji wa *Wimbo Ulio Bora* ambaye mara kwa mara hukutana na jazanda katika vifungu mbalimbali vya wimbo huu wa kimapenzi.

Barton (1998:21) anasema kuwa karne ya ishirini imeshuhudia jambo la kuvutia kwa Biblia kuonekana kama kazi ya kifasihi. Mtazamo huu hutokana na ukweli kwamba Biblia ni mkusanyiko wa matini zilizoandikwa kisanaa kama vile hadithi, ushairi na barua.

Katika utafiti huu, ni vigumu kujiepusha na kuziangalia jazanda za *Wimbo Ulio Bora* kwa mtazamo huo wa kisanaa kwa sababu jazanda ni mojawapo wa mbinu zitumiwazo na wasanii kulinganisha vitu viwili kwa misingi ya sifa zinazofanana. Maoni haya yatatusaidia katika kazi hii kwani yatatuongoza kukisia maana zilizolengwa na mwandishi katika jazanda husika.

Barton (1998:129) anadai kwamba, Biblia kama maktaba ya kazi za kifasihi iliyoandikwa kwa lugha tatu asilia ambazo ni Kihebrania, Kiaramaiki na Kigiriki na kutafsiriwa katika lugha zaidi ya elfu mbili, bila shaka hupigiwa maswali na wanaisimu katika viwango vya utekelezaji na vya kinadharia (practical and theoretical levels). Wengi wa wafasiri wa Biblia huyakabili maswali haya kwa msingi wa kipragmatiki. Maoni haya ya wafasiri wa matini za Biblia ni hazina muhimu kwa muradi huu kwa vile msingi wetu mmoja wa nadharia uliotuongoza ni ule utumiwao na wengi wa wafasiri wa Biblia; nadharia ya Pragmatiki ya Grice (1967). Rejelea sehemu ya 2.2.2 kwa maelezo zaidi.

Danielson katika *Word of God*: 455), asisitiza kuwa, aghalabu kuna fasiri nyingi za Biblia kama kulivyo na makundi mengi ya kidini au hata watu binafsi. Kutokana na haya, je, inawezekana kufahamu maana sahihi ya kifungu mahsusi cha Biblia? Kwa kweli moyo wa mtafuta ukweli unalia pamoja na mhubiri katika kitabu cha Mhubiri 8:1, palipoandikwa kwamba: 'Ni nani aliye kama mwenye hekima; Naye ni nani ajuaye kufasiri neno? Maoni haya yanaturejesha nyuma katika mada yetu ya utafiti. Hili ni dhihirisho tosha kwamba kunao utofauti katika kufasiri matini za Biblia. Jambo hili pia linampa mtafiti msukumo wa kuchunguza nafasi ya mbinu ya jazanda katika *Wimbo Ulio Bora*. Je, inawezekana kuwa utofauti katika ufasiri wa wimbo huu hutokana na utata ulioko kwenye jazanda hasa katika vifungu ambamo mbinu hii imetumika? Utafiti huu utatuwezesha kujibu swali hili kwa uhakika.

Imbosa (1990) amehakiki jazanda katika Ushairi wa Muyaka kama mbinu ya kisanaa. Kazi yake inafanana na hii yetu kwani mbinu tunayoifasiri ndiyo ile aliyoihakiki. Tofauti ni kwamba kazi yetu inafasiri jazanda kwa mikabala ya kidini na kijamii ilhali yeye alichunguza jazanda kama mbinu ya kishairi.

Tofauti nyingine ni kwamba, Imbosa alichunguza matumizi ya jazanda katika Ushairi wa Muyaka ilhali sisi tunachunguza jazanda katika *Wimbo Ulio Bora*. Hata hivyo, kazi yake imetufaa sana kwani imetuwekea msingi bora wa kuielewa dhana ya jazanda kwa upana.

Istilahi tofauti zimetumika na wataalamu mbalimbali kumaanisha jazanda. Hali hii inaonyesha kuwa kuna utata hata katika kijelezi cha jazanda. Hata hivyo, ingawa wataalamu mbalimbali wanatumia istilahi tofauti tofauti kumaanisha jazanda, kuna maelezo fulani ambayo wanakubaliana kuwa yanafafanua dhana hii.

Mazrui (1981:2) ameeleza jazanda na istiari kama mbinu za lugha zenye maana sawa. Kwake mazrui, jazanda au istiari ni fumbo linalohitaji kufumbuliwa. Chacha (1987) katika Imbosa (1990:15), amefafanua istiari kuwa kitu kilichosetiriwa, kilichofumbwa ili undani wake ufumbuliwe. Kutokana na ufafanunzi wa Mazrui na Chacha, jazanda na istiari zina maana sawa kwa kuwa zinalenga jambo lililofichwa ambalo linahitaji kufumbuliwa.

Kulingana na Mulokozi na Kahigi (1979), sitiari ni tamathali ambayo athari yake hutegemea uhamishaji wa maana kutoka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Vitu viwili vinavyofananishwa huwa havina uhusiano wa moja kwa moja. Wanachosisitiza Mulokozi na Kahigi ni hali ya uhamisho. Tunanaweza kuchukulia kuwa ikiwa kutatokea maelezo yoyote ambamo hamna uhamisho wa maana, basi hiyo si jazanda. Katika utafiti huu, maoni haya yanadhihirika kupitia mwongozo wa Leech (1969) wa kupambanulia jazanda – rejelea sehemu ya 2.2.1.

Senkoro (1982) ametumia sitiari kumaanisha mbinu ya lugha ambayo hulinganisha vitu ama watu lakini bila kutumia viunganishi linganishi. Kwa hivyo, "sitiari" ya Senkoro na ya Mulokozi na Kahigi itakuwa na maana sawa na "istiari" ya Chacha na Mazrui

Kulingana na Imbosa (1990:16), wataalamu wengi wanakubaliana kwamba tunapozungumza juu ya jazanda, tunafikiria kuhusu uhusiano kati ya vitu viwili au maelezo aina mbili; A na B. Maelezo au sifa za B zinahamishwa kwa A. Kwa hivyo, A inazungumziwa kama kwamba ni B.

Kufikia hapa tunatilia maanani kuwa jazanda ni fumbo na ili tuitambue mbinu hii, lazima kuwe na hali ya "uhamisho" wa maana kwa kuwa ndiyo inaleta dhana ya "fumbo". Leech (1969) anasema kuwa kila mhakiki ana uhuru wa kuzitolea jazanda fasiri yake bora tu asikiuke mipaka ya miktadha.

Kwa muhtasari, tumedokeza mambo muhimu ambayo tumezingatia katika kufasiri jazanda za *Wimbo Ulio Bora*. Mambo hayo ni kama yafuatavyo:

1. Jazanda ni fumbo linalohitaji kufumbuliwa.
2. Kuna swala la uhamishaji wa maana katika matumizi ya jazanda.
3. Ili kufasiri jazanda, mfasiri sharti aelewe umuhimu ulioko kati ya kizungumzwa, kifananishi na kiungo.
4. Kila mfasiri anaweza kuuwekea mipaka uchambuzi wake wa jazanda, bora tu asikiuke mipaka ya miktadha.

**2.2 Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na misingi mitatu ya nadharia. Mwongozo wa Leech (1969) wa kupambanua jazanda ulituongoza kutambulisha vitu vinavyofananishwa katika jazanda za *Wimbo Ulio Bora* na hivyo basi kuweza kubaini maana ya kijuu juu na hatimaye maana ya ndani.

Nadharia ya Pragmatiki ya Grice (1967) ya kuhesabu vidokezi katika mazungumzo/maandishi ilitusaidia kueleza sababu za utata katika jazanda za *Wimbo Ulio Bora.* Tulijikita katika Kaida ya Ushirikiano ambapo tulichunguza kanuni zilizokuwa zimevunjwa ili kuzua maana mbalimbali kwa mikabala ya kidini na kijamii.

Ili kudhihirisha jinsi jazanda za kidini za *Wimbo Ulio Bora* zinavyoweza kutumika katika miktadha ya kijamii, tuliongozwa na vipengele vya akronimu ya MWALEKIHAMKANYA (SPEAKING) ya Hymes (1974) katika nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano.

### 2.2.1 Uainishaji wa Leech

Leech (1969), huku akiungwa mkono na Mulokozi na Kahigi (1979), wanakubaliana kwamba jazanda ina sehemu tatu muhimu:

- Kizungumzwa
- Kifananishi
- Kiungo

Leech (1969) ameainisha hatua za kupambanua jazanda katika kazi ya msanii. *Wimbo Ulio Bora* haujitengi na uainishaji huu kwa sababu pia umeandikwa kisanaa.
Ushairi uliomo pamwe na matumizi ya mbinu za kifasihi kama vile jazanda, tashbihi na chuku yanathibitisha kauli hii. Katika kupambanua jazanda, Leech alipendekeza hatua tatu zifuatazo:

Hatua ya I - Kutenganisha maana ya juu na maana ya ndani. Mhakiki aamue ni ipi maana ya juu na ni ipi maana ya ndani.

Hatua ya II - Mhakiki afahamu na kutenganisha kizungumzwa na kifananishi.

Hatua ya III - Mhakiki atambue kiungo. Ili kutambua kiungo, maana ya juu na ile ya ndani ni lazima zibainishwe.

Sentensi ifuatayo inamhusu aliyekuwa waziri wa Serikali za Wilaya nchini Kenya kati ya mwaka wa 2003 na 2004, marehemu mheshimiwa Karisa Maitha.

(12): "Karisa Maitha alikuwa kimbunga". (Mfano huu ni wangu).

Mtu anaposema kuwa Karisa Maitha alikuwa kimbunga, ana maana kwamba Maitha alikuwa nazo sifa au tabia ambazo kwa kawaida tungezihusisha na kimbunga (upepo wenye nguvu nyingi). Katika mfano huu, kizungumzwa ni Karisa Maitha ilhali kifananishi ni kimbunga. Kiungo ni zile sifa za kimbunga kwa mfano kwenda kasi, kuvuma kwa nguvu na uharibifu. Kwa hivyo, jazanda ya Karisa Maitha kuwa kimbunga inatumika kama lugha ya mkato ambayo kwa fumbo inatueleza mengi kuhusu kizungumzwa; Karisa Maitha. Kama alivyosema Mulokozi (1979), ujumbe tuupatao kutoka kwa sitiari (jazanda), sio wa kimawazo tu bali pia ni wa kihisia.

Katika mfano wa (12), hisia tulizonazo kuhusu kimbunga zinahamishwa kwa Karisa Maitha.

Aidha, mhakiki ajiulize maana ya juu na ya ndani zitalinganishwa kwa kushikilia kigezo kipi. Ikisemwa Maitha alikuwa kimbunga, tutalinganisha Maitha na kimbunga kwa kigezo kipi? Je, ni kasi, uvumaji au uharibifu? Bila shaka ni uvumaji. Popote Karisa Maitha alipokwenda katika maeneo ya wizara yake, kila mfanyakazi alifahamu kwani waziri huyu aliendda kwa kishindo kikuu - alikuwa mtenda kazi hasa!

Tunafahamu kuwa katika kufafanua jazanda za wimbo huu, uainishaji huu wa Leech ulitufaa sana kwa sababu ulitupa msingi bora wa kutenganisha jazanda na lugha ya kawaida.

(13): Mimi ni ua la uwandani (2:la)

- Kizunguzwa – Msichana wa kijijini au mashambani (Mshulami).
- Kifananishi – Ua lililo uwandani/kondeni au uwanjani.
- Kiungo – Ua kutofichika na kuvutia macho.
- Maana ya kijuu juu – Msichana/mwanamke mwenye uzuri/urembo unaovutia wanaume wengi (uzuri/urembo usiofichika).
- Maana ya ndani – Mungu aliyejaa uzuri usiofichika.

### 2.2.2 Pragmatiki ya Grice

Grice (1967) anapendekeza Kaida ya Ushirikiano katika jitihada za kuelezea jinsi maana ya mzungumzi huzuka. Kaida ya Ushirikiano inasema kwamba; "Zungumza kama inavyostahili, mahali panapostahili, kwa nia inayokubalika na mwelekeo wa mazungumzo ambapo wewe unahusika". (Thomas 1995:61).

Kaida hii ya Ushirikiano hubeba kanuni nne:

Kiasi 1. Hakikisha habari unayotoa inafahamisha kama vile inavyostahili.

2. Usitoe habari inayofahamisha zaidi ya vile inavyostahili.

Thamani 1. Usiseme yale unayoamini kuwa uongo.

2. Usiseme yale ambayo hauna ithibati ya kutosha.

| | |
|---|---|
| Uhusiano | Zungumza yale tu yanayohusiana na mada. |
| Namna | 1. Jiepushe na utani unaoweza kukufanya usieleweke.<br>2. Jiepushe na utata.<br>3. Tumia maelezo mafupi.<br>4.Tumia mpangilio mzuri.<br>(Thomas 1995:63) |

Kanuni hizi zinaelekeza yale yanayopasa kufanywa na washiriki ili wazungumze kwa njia inayoeleweka kwa urahisi. Wanapaswa kuzungumza ukweli, kuzingatia mada iliyopo, kuwa wazi huku wakitoa habari kamili; Levinson (1992:102). Kaida ya Ushirikiano na kanuni zake zilitumiwa katika utafiti huu kama msingi wa kurejelea vidokezi; fasiri za nia ya kimawasiliano za mzungumzi zaidi ya maana ya kisemantiki katika matini ya *Wimbo Ulio Bora*. Kulingana na Grice, vidokezi vya maana vinanaweza kuundwa kwa kuvunja kanuni za ushirikiano. Tulitathmini na kisha kuamua kanuni zilizokiukwa katika kila jazanda za *Wimbo Ulio Bora*.

Ifuatayo ni sehemu ya mazungumzo yaliyofanywa na Mfalme wa jamii ya Matebele kwa Malkia Viktoria:

(14): "Mimi ni chawa katika ukingo wa blanketi ya jalalati Malkia".
(Thomas1995: 89).

Mzungumzi (mfalme) hapa anazua kidokezi kwa kuvunja kanuni ya "namna" (kwa kutumia tamathali ya semi). Anamaanisha kuwa, yeye si chochote wala lolote akilinganishwa na Malkia. Hata hivyo, yawezekana kuwa mfalme anamaanisha yafuatayo:

i) Matandiko ya Malkia ni machafu:

ii) Usafi wa Malkia unatia shaka.

Maoni haya ni muhimu katika utafiti huu kwani jazanda moja inaweza kufasiriwa kwa njia mbalimbali ili kukidhi haja za miktadha tofauti tofauti.

Nadharia hii inayohusu kuhesabu vidokezi katika mazungumzo ilitusaidia katika uchanganuzi wa Data. Kulingana na nadharia hii ya Pragmatiki, ya Grice (1967), watu huelewana katika mazungumzo kwa sababu ya kuzingatia Kaida ya Ushirikiano. Endapo mojawapo au kanuni zote zinazojenga kaida hii zitakiukwa, utata wa maana ya ujumbe huzuka na hivyo kuufanya ujumbe huo kueleweka kwa njia mbalimbali au kutoeleweka kamwe. Kwa mfano katika jazanda ifuatayo, tulichunguza kanuni zilizokuwa zimevunjwa na hivyo kupelekea kutumia vidokezi vya maana:

(15): Mimi ni ua la uwandani (2:1a)

- Kiasi – Habari iliyotolewa katika jazanda hii haitoshi kufahamisha kama inavyostahili. Mshulami anapodai kuwa yeye ni ua la uwandani, haieleweki moja kwa moja maana aliyoikusudia. Kwa hivyo, kanuni hii imevunjwa hali ambayo inasababisha utata wa kimaana.

- Thamani – Utoaji wa habari za ukweli ndilo jambo muhimu katika kanuni hii. Hata hivyo, Mshulami anapodai kuwa yeye ni ua la uwandani, si rahisi kung'amua moja kwa moja anachomaanisha. Matumizi haya ya mafumbo yanasababisha utata wa maana. Kanuni hii imekiukwa.

- Uhusiano – Jambo muhimu katika kanuni hii ni utoaji wa habari zinazohusiana na mada. *Wimbo Ulio Bora* ni wimbo wa mapenzi. Jazanda hii ni ya kimapenzi. Kwa hivyo, kanuni hii haijavunjwa; imezingatiwa.

- Namna – Kipengele muhimu cha uelewekaji katika mazungumzo hakijazingatiwa. Hii ni kwa sababu, badala ya kujiepusha na utata, msemaji anatoa kauli inayotatanisha hususan kwa kutumia fumbo. Habari tunazopata katika jazanda hii hazituelekezi kung'amua moja kwa moja ni kwa misingi ipi Mshulami akawa ua la uwandani. Kanuni hii imevunjwa.

### 2.2.3 Ethnografia ya Mawasiliano

Nadharia hii iliasisiwa na Hymes (1974). Inajikita katika Anthropolojia na Isimu. Kulingana na nadharia hii, matumizi ya lugha katika hali mbalimbali ya mazungumzo husaidia katika kuelewa tamaduni za washiriki. Hymes alipendekeza kuwa matumizi ya lugha ni matukio ambamo uneni hutendeka.

Hali hii aliiita tukio la uzungumzi au tukio neni. Basi, tamko lolote hutokea katika tukio na kwa upande mwingine, vitendo hutokea katika matukio. Sio malengo ya utafiti huu kuchunguza tamaduni za washiriki katika matini ya *Wimbo Ulio Bora* bali ni kuchunguza miktadha ya uzungumzi. Hata hivyo, msingi aliopendekeza Hymes katika Thomas (1995:18) ndio ulikuwa muhimu sana kwetu.

Hymes alipendekeza njia inayoweza kutumika katika kuelewa mazungumzo. Alifanya hivyo kwa kubuni akronimu aliyoiita SPEAKING - MWALEKIHAMKANYA ambapo kila herufi husimamia kipengele maalum kinachotumika katika mazungumzo.

S (M) - Setting (Mandhari).
P (WA) - Participants (washiriki).
E (LE) - Ends (Lengo/malengo).
A (KI) - Act Sequence (s) (Vitendo).
K (HA) - Key (Hali).
I (M) - Instrumentalities (Msimbo).
N (KA) - Norms of Interaction and Interpretation (Kaida).
G (NYA) - Genre (Nyanja).

Kwa kutumia vipengele hivi, tuliweza kuchunguza miktadha ya kijamii ambamo jazanda za wimbo huu zinaweza kutumika. Vipengele ambavyo hasa vilituongoza katika nadharia hii ni mandhari, washiriki, lengo, kitendo/vitendo, hali, msimbo na nyanja. Nadharia hii ilitusaidia hasa katika uchanganuzi wa Data.

(16): "Mimi ni ua la uwandani" (2:1a):

Mandhari – Kondeni au uwanjani au mashambani.
Washiriki – Mwanaume na mwanamke (Sulemani na Mshulami).
Lengo – Kuusifu uzuri/urembo wa msichana wa kijijini.
Vitendo – Masimulizi ya uzuri wa msichana wa kijijini.
Hali – Furaha, upendo na ushawishi.
Msimbo – Lugha ya mafumbo katika dini.
Nyanja – Wimbo wa mapenzi unaotumiwa kufumba uzuri wa Mungu.

## SURA YA TATU

## NJIA ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Utafiti huu ulikuwa wa kipekuzi. Kwa hivyo, utafiti wetu ulifanywa kwa wingi kiambatishoni. Utafiti wenyewe ulilenga matumizi ya jazanda katika *Wimbo Ulio Bora*. Kusoma Biblia hasa *Wimbo Ulio Bora* na miongozo mbalimbali ya Biblia, kutambulisha jazanda na kuzinukuu ndizo mbinu tulizotumia katika ukusanyaji wa Data. Hizi mbinu ndizo zilizotusaidia kupekua yaliyomo katika matini yetu. Katika sura hii, tunaonyesha jinsi tulivyoiteua sampuli, tulivyoikusanya Data na kuichanganua huku tukiongozwa na mihimili katika kila nadharia zilizouongoza utafiti huu.

### 3.2 Historia ya Chimbuko la *Wimbo Ulio Bora*

Kama tulivyokwishataja katika Sura ya Pili (2.2) kwenye tasnifu hii, *Wimbo Ulio Bora* ni kitabu cha 22 kati ya vitabu 39 vya Agano la Kale katika Biblia. Kuhusu uandishi wa wimbo huu, matoleo tofauti tofauti ya Biblia yanaafikiana kwamba mwandishi ni Mfalme Sulemani. Biblia zote zinatufungulia wimbo huu kwa maneno yafuatayo katika *Wimbo Ulio Bora*, Sura ya Kwanza na msitari wa Kwanza:

"*Wimbo Ulio Bora*, wa Sulemani".

Kulingana na utamaduni wa Waebrania, Sulemani alikuwa mtunzi wa nyimbo. Kwa sababu hii, " wimbo ulio mkuu kuliko zingine" ulihusishwa naye kama ilivyo bayana katika 1:1. Haya ni kwa mujibu wa *The New Jerusalem Bible* (1985:1027). Umaarufu wake wa kutunga nyimbo ulikuwa karama kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Katika Wafalme wa Kwanza, 5:12, tunaarifiwa kwamba:

"Bwana akampa Sulemani hekima, kama alivyomwahidia".

Hekima aliyopewa Sulemani na Mungu ilimfanya awe maarufu sana duniani na kwamba hakuna mtu mwingine aliyewahi kuwa mwenye hekima kama yeye. Habari tunazopata katika kitabu cha Wafalme wa Kwanza, 4:29-34, zinaangazia swala hili kwa uwazi zaidi kama ifuatavyo:

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

> 29 Mungu akampa Sulemani hekima, na akili nyingi sana,
> na moyo mkuu,kama mchanga ulioko Pwani. 30 Hekima ya
> Sulemani ikapita hekima ya wana wote wa Mashariki, na
> hekima zote za Misri. 31 Kwa kuwa alikuwa na hekima kuliko
> watu wote; kuliko Ethani Mwezrahi, na Hemani, na Kalkoli,
> na Darda,wana wa Maholi; zikaenea sifa zake kati ya
> mataifa yote yaliyozunguka. 32 Naye akanena mifano elfu
> tatu, na nyimbo zake zilikuwa elfu moja na tano. 33 Akanena
> habari za miti tangu mwerezi ulioko Lebanoni hata hisopo
> umeao ukutani; pia akanena habari za wanyama, na za ndege,
> na vitambaavyo, na samaki. 34 Wakaja wa mataifa yote ili
> waisikie hekima ya Sulemani, toka wafalme wote wa
> ulimwengu, waliokuwa wamepata habari za hekima yake.

Kutokana na kifungu hiki, hususan msitari wa 32, madai kuwa Sulemani alikuwa mtunzi wa nyimbo si uongo! Aliandika jumla ya nyimbo 1005 na hivyo *Wimbo Ulio Bora* ni mmoja tu kati ya nyimbo hizo. Licha ya Biblia, Miongozo ya ufasiri wa Biblia pia imemthibitisha Sulemani kuwa mwandishi wa wimbo huu. Miongozo hii ni pamoja na *The New Jerusalemu Bible* (1985:1027), *The Holy Bible Concordance* (1979:705), *Explore The Book in One Volume; Volume Three* (1973:171), *The NIV Study Bible* (1995) na *The Interpreter's Bible; Volume 5.* (1978:91).

Kuhusu tarehe ya uandishi, Scofield (1979:705) anasema kuwa wimbo huu uliandikwa karne ya Kumi Kabla ya Kristo. Akifafanua anwani "*Wimbo Ulio Bora*", Barker (1995:997 anasema kuwa anwani hii katika matini ya Kiebrania ni *Wimbo wa Sulemani* kumaanisha aidha mojawapo ya mambo haya matatu:

1. Wimbo ulioandikwa na Sulemani.
2. Wimbo wa Sulemani.
3. Wimbo kuhusu Sulemani

Kwa maoni yetu, tumehitimisha kwamba anwani "*Wimbo wa Sulemani*" inamaanisha kuwa huu ni wimbo ulioandikwa na Sulemani. Tumetoa kauli hii kutokana na marejeleo tuliyoyasoma ambayo kwa pamoja yalikubaliana kuhusu uandishi wa Sulemani wa wimbo huu. Mbali na *Wimbo Ulio Bora*, Sulemani pia aliandika vitabu vya Mithali na Mhubiri.

Sulemani alitunga wimbo huu kumrejelea Mungu. Sulemani aliishi katika kipindi ambapo kuabudu sanamu na miungu haikuwa kioja. Alikuwa tajiri mkubwa wa enzi hiyo; (Wafalme wa Kwanza, 10:14-29). Aidha, alikuwa mwenye hekima nyingi ambayo ilimtwika sifa mno; (Wafalme wa Kwanza, 4:29-34). Kutokana na utajiri wake, ingekuwa rahisi kumpuuza Mungu huku akiiabudu mali yake. Vilevile, ingekuwa rahisi kumsahau Mungu kwa sababu ya sifa nyingi alizokuwa nazo kutokana na hekima yake kuu. Kama mfalme, haingekuwa ajabu kwake kutomweka Mungu mbele. Hata hivyo, sifa hizi hazikumfunga Sulemani macho asimtambue Mungu. Katika kila jambo, alikumbuka kumweka Mungu mbele kwani ndiye aliyemweka katika kiti cha kifalme (Wafalme wa Kwanza, 2:24).

Mambo haya yanatuonyesha jinsi Sulemani alivyompenda Mungu. Ithibati inayotudhihirishia jinsi Sulemani alivyomhusudu Mungu, ni ujenzi wa hekalu (Wafalme wa Kwanza, 6:1). Tunashawishika kwamba, hangejihusisha na muradi mkubwa kiasi hicho na wenye gharama kubwa iwapo aliyemjengea hekalu hakumthamini kwa vyovyote vile. Ili kudhihirisha mapenzi yake kwa Mungu, Sulemani alichagua kumtungia Mungu wimbo kwa kutumia hekima nyingi aliyomtunukia. Tajriba imeonyesha kwamba, maneno yaliyowekwa katika wimbo hunata akili kuliko maneno ya kinatharia. Maneno/habari husemeka kwa urahisi yawapo katika wimbo. Aidha, katika wimbo huwa kuna burudani. Sulemani aliyafahamu yote haya na ndipo akaamua kumsifu Mungu wake kupitia kwa uimbaji. Kwa mfano, anapomrejelea Mungu kama "Ua la Uwandani" katika (2:1a), anatuchorea picha ya upendo au mapenzi. Kwa jumla, ua huashiria mapenzi na kupendwa. Ua huvutia kwa sababu ya rangi yake na pengine harufu inayonukia vizuri. Basi, Sulemani anampenda Mungu wake sana mithili ya jinsi maua yanavyopendwa na watu.

### 3.3 Uteuzi wa Sampuli

Ni dhahiri kwamba wanafasihi wengi hutumia mbinu ya jazanda kwa wingi kuendeleza maudhui yao. *Wimbo Ulio Bora* ni kitabu cha kidini ambacho sawa na kazi nyingine za kifasihi, kimetumia jazanda kuendeleza maudhui yake. Kitabu hiki kimeandikwa kwa njia ya kishairi. Vitabu vingine vya kishairi ni Ayubu, Zaburi, Mithali na Mhubiri.

Hata hivyo, jazanda za kimapenzi zilizomo katika *Wimbo Ulio Bora* pamoja na kuunyima wimbo huu viashiria vya kidini kwa mfano 'Mungu', ni hali inayozua utata wa kifasiri. Hii ndiyo sababu jazanda zake zinaweza kufasiriwa kwa mikabala ya kidini na kijamii. Basi, uteuzi ulikuwa wa kimakusudi kwani ingechukua muda mrefu na gharama kubwa endapo tungehusisha vitabu vyote vitano vya kishairi katika utafiti huu.

**3.4 Ukusanyaji wa Data**

Data yetu ni jazanda zilizomo katika *Wimbo Ulio Bora*. Jazanda hizo zilipatikana kwa kuusoma wimbo wote katika matoleo mbalimbali ya Biblia pamoja na miongozo anuwai ya Biblia. Kwa jumla, tulihusisha jazanda ishirini na tano kama zilivyojiri sura baada ya nyingine. Orodha ifuatayo ya jazanda inathibitisha haya.

- Mimi ni mweusi-mweusi, lakini
  ninao uzuri.
  (1:5a).
- Enyi binti za Yerusalemu, (1:5b).
- Jua limeniunguza (1:6a).
- Wana wa mamangu (1:6b).
- Mlinzi wa mashamba ya mizabibu (1:6c).
- Mimi ni ua la uwandani (2:1a).
- Mimi ni nyinyoro ya mabondeni (2:1b)
- Hua wangu, mafichoni mwa Jabali
  Katika sitara za magenge,
  Nitazame uso wako, nisikie sauti yako
  Maana sauti yako ni tamu na uso wako mzuri
  (2:14).

- Tukamatie mbweha,
  Wale mbweha wadogo,

- Waiharibuo mizabibu,
  Maana mizabibu yetu
  yachanua.
  (2:15)

- Bustani iliyofungwa ni umbu
  langu, bibi arusi, (4:12a).

- Kijito kilichofungwa, (4:12b).
- Chemchemi iliyotiwa muhuri.(4:12c)

- Machipuko yako ni bustani ya
  komamanga,
  Yenye matunda mazuri. hina
  na nardo
  (4:13)

- Wewe ndiwe chemchemi ya
  bustani yangu,

- Kisima cha maji yaliyo hai.
  Vijito vya Lebanoni viendavyo
  Kasi
  (4:15b).

- Wako malkia sitini, na masuria
  themanini,
  Na wanawali wasiohesabika;

- Hua wangu, mkamilifu wangu, ni
  mmoja tu,
  Mtoto wa pekee wa mamaye.
  (6:8-9)

- Mwako wake ni mwako wa moto, (8:6e).

- Na miali yake ni miali ya
  Yahu.
  (8:6f).

- Mimi nalikuwa ukuta,
  Na maziwa yangu kama minara;

- Ndipo nikawa machoni pake
  Kama mtu aliyepata amani.
  (8:10).
- Shamba langu la mizabibu, lililo
  langu mimi, li mbele yangu.
  (8:12a)

**3.5 Uchanganuzi wa Data**

Jazanda zilizomo katika wimbo huu zilifafanuliwa katika mikabala ya kidini na kijamii. Kisha ilidhihirishwa jinsi jazanda za *Wimbo Ulio Bora* japokuwa ni za kidini, zinavyoweza kutumika katika miktadha ya kijamii. Maelezo yalitolewa kuhusiana na fasiri zilizopatikana na ufaafu wazo katika miktadha mahsusi ya kijamii. Ili kufanikisha uchanganuzi wa data, sehemu tatu zifuatazo zilituongoza kupambanua jazanda na kuziweka wazi:

a) Hatua za upambanuzi kulingana na Leech (1969):

i. Kutenganisha maana ya kijuu juu na maana ya ndani ya kila jazanda.

ii. Kutenganisha kizungumzwa na kifananishi katika kila jazanda.

iii. Kutambua kiungo katika kila jazanda.

b) Vipengele vya Pragmatiki ya Grice (1967):

Kaida ya Ushirikiano katika mawasiliano hujengwa juu ya kanuni nne ambazo ni:

(i) Kiasi.

(ii) Thamani.

(iii) Uhusiano.

(iv) Namna.

Tulitathmini kanuni zilizokuwa zimevunjwa katika kila jazanda. Msingi hapa ni kwamba, uvunjaji wa kanuni hizi huasi Kaida ya Ushirikiano; hali ambayo huzua utata katika kubaini maana iliyokusudiwa na mzungumzi au mwandishi. Utafiti wetu ulitufichulia kwamba, jazanda za *Wimbo Ulio Bora* zinaweza kutumika katika miktadha ya kijamii. Jambo hili linatokana na uvunjaji wa kanuni zinazounda Kaida ya Ushirikiano hasa 'kiasi' na 'namna'.

c) Vitengo vya Akronimu ya Hymes (1974):

Ili kudhihirisha jinsi jazanda za kidini za *Wimbo Ulio Bora* zinavyoweza kutumika katika miktadha ya kijamii, tuliongozwa na msingi wa nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano kulingana na maoni ya Hymes (1974). Vitengo vya akronimu ya Hymes ambavyo hasa vilituongoza kufikia madhumuni haya ni:

i) Mandhari.

ii) Washiriki.

iii) Lengo/Malengo.

iv) Vitendo.

v) Hali.

vi) Msimbo.

vii) Nyanja.

### 3.6 Hatua za Kuchanganulia Jazanda kutokana na Misingi ya Nadharia

Kutokana na misingi ya nadharia tulizochagua, tulijenga mpango au hatua za kuchanganulia kila jazanda zilizomo katika *Wimbo Ulio Bora*. Hebu tuchukue jazanda moja kama mfano wa jinsi mpango huu ulivyotuongoza katika uchanganuzi wa Data.

(17): Mimi ni ua la uwandani

A. Kutambulisha vitu vinavyofananishwa kutokana na mwongozo wa Leech (1969).

- Ua la uwandani linafananishwa na msichana wa kijijini.
- Kutoa maana ya kijuu juu - Ua la uwandani ni msichana mrembo/mzuri asiyefichika.

B. Kufuatia akronimu ya MWALEKIHAMKANYA ya Hymes (1974), tulizingatia vipengele vifuatavyo ili kudhihirisha jinsi jazanda za kidini za *Wimbo Ulio Bora* zinavyoweza kutumika katika miktadha ya kijamii.

- Mandhari – Kondeni, uwanjani.
- Washiriki – Sulemani na Mshulami.
- Lengo – Kuonyesha uzuri/urembo usiofichika wa msichana.
- Vitendo – Masimulizi ya uzuri wa msichana.
- Hali – furaha na upendo.
- Msimbo – Lugha ya mafumbo katika dini.
- Nyanja – Wimbo wa mapenzi unaotumika kufumba uzuri wa Mungu.

C. Ili kubaini chanzo cha utata wa ufasiri wa jazanda zilizomo katika *Wimbo Ulio Bora*, tulizingatia kanuni za Kaida ya Ushirikiano katika mawasiliano kulingana na Pragmatiki ya Grice (1967).

- Kiasi – Kanuni hii inasisitiza kwamba habari inayotolewa katika mazungumzo, inafaa kufahamisha kama inavyostahili na aidha isifahamishe kuliko inavyotarajiwa. Katika mfano wetu wa jazanda ya "mimi ni ua la uwandani" (2:1a), kuna upungufu katika kiwango cha ufahamishaji. Habari iliyotolewa haitoshi kufahamisha kile kilicholengwa na msemaji (Mshulami). Kwa hiyo, kanuni hii imevunjwa hali inayopelekea ukiukaji wa Kaida ya Ushirikiano.

- Thamani – Kanuni hii hutilia mkazo utoaji wa habari za ukweli. Mshulami anapokiri kwamba yeye ni ua la uwandani, hakuna ukweli wa moja kwa moja kuwa yeye ni ua la uwandani na hivyo kuivunja kanuni hii. Basi, inatubidi tuurejelee mwongozo wa Leech (1969) wa ulinganishaji wa vitu vyenye sifa zinazofanana ili tupate maana ya kijuu juu.

- Uhusiano – Kanuni hii inasisitiza utoaji wa habari ambazo zinahusiana na mada peke yake. Mada inayozungumziwa katika *Wimbo Ulio Bora* ni mapenzi. Mshulani anaposema kuwa yeye ni ua la uwandani kwa Sulemani, inatubidi turegelee nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ambapo tuligundua kwamba maneno haya yalisemwa katika hali ya furaha na upendo. Kwa hivyo, kanuni ya uhusiano umezingatiwa na Kaida ya Ushirikiano haijavunjwa kwa ambavyo yanayosemwa yanahusiana na mada ya kimapenzi moja kwa moja.

- Namna – Kanuni hii inatilia mkazo uwazi na uelewekaji wa habari zilizotolewa katika mazungumzo. Katika mfano wa "mimi ni ua la uwandani", msemaji amezingatia ushauri wa Grice (1967) katika Levinson (1992:102) na Grundy (2000:75) wa kutumia maelezo mafupi pamoja na mpangilio mzuri katika mazungumzo. Hata hivyo, kipengee muhimu cha 'uelewekaji' hakijazingatiwa ambapo badala ya kujiepusha na utata, msemaji anatoa kauli inayotatanisha. Haieleweki ni kwa misingi ipi msemaji awe ua la uwandani. Hali hii inatufanya turegelee mwongozo wa Leech (1969) ambao unatuongoza katika kufananisha msichana wa kijijini na ua la uwandani. Aidha, kutokana na utata unaozuka, inatubidi turegelee mwongozo wa Hymes (1974) wa MWALEKIHAMKANYA. Mandhari inayojitokeza katika jazanda hii ni ya mashambani ambapo kuna konde au uwanja. Washiriki ni mwanaume na mwanamke (Sulemani na Mshulami), lengo ni kuonyesha uzuri usiofichika ilhali kuna hali ya furaha na upendo.

D. Kutoa maana ya ndani:

(i) Ya kidini – Wimbo huu ni aina ya mazungumzo kati ya wapenzi wawili; Sulemani na Mshulami. Katika jazanda hii, anayezungumza ni Mshulami. Anaonekana hapa akijaribu kuyateka mawazo ya Sulemani kwa kumjulisha vile yeye msichana alivyo mzuri/mrembo. Anatumia taswira ya vitu ambavyo Sulemani kama rafiki yake anavijua kutokana na mazingira alimokulia. Hapa anamwambia kuwa yeye msichana ni kama ua la uwandani ambalo huonekana na watu wote; huvutia macho mengi. Kuna wanaume wengi wanaomtamani kutokana na uzuri wake. Kwa kusisitiza uzuri wake, anaendelea kumwarifu mpenzi wake Sulemani kwamba yeye ni nyinyoro ya mabondeni ambayo hainyauki kwani kuna unyevu nyakati zote bondeni. Mapenzi yake kwa Sulemani hayapungui. Maana ya ndani ya kidini ni kwamba Mungu anafananishwa na Mshulami ambaye ni msichana mzuri/mrembo sana; hakuna mwingine aliyefikia uzuri wake (ni mtoto wa pekee wa mama yake).

Kupitia jazanda hii, Sulemani anatuchorea picha ya uzuri wa Mungu wake; Mungu ambaye ni mwingi wa wema/uzuri. Kutokana na yale yaliyoelezwa hapo juu (3.6; A-C) kwa misingi ya Leech (1969), Hymes (1974) na Grice (1969), maana ya ndani ya kidini ya " ua la uwandani" ni Mungu anayefananishwa na ua.

Kwa kawaida, ua huashiria upendo au mapenzi. Jinsi watu wanavyoyapenda maua, ndivyo Sulemani anavyompenda Mungu kiasi cha kumlinganisha na ua hasa la uwandani ambalo huvutia macho mengi. Hali ya upendo na furaha tuliyoibaini kutokana na nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano ya Hymes (1974) inadhihirisha haya.

(ii) Ya kijamii - Maana ya ndani ya kijamii ya jazanda hii ni binti anayejitapia urembo wake kwa nia ya kumteka mwanaume rafiki yake kimapenzi. Kwa mfano wakati wa utongozaji ambapo washiriki huwa mwanaume na mwanamke huku hali ikiwa ya upendo, furaha, usnawishi na matarajio makuu.

Binti anaweza kumfumbia rafiki yake mwanaume jazanda hii kwamba yeye (msichana) ni "ua la uwandani" kwa lengo la kuusifu uzuri na urembo wake usiofichika. Kutofichika kwa uzuri wake kuna maana kwamba mwanaume huyo asipozinduka na kuchukua hatua mapema ya kumchukua msichana huyo, anaweza akaambulia patupu kwani kuna wanaume wengine wengi wanaomtamani sana.

# SURA YA NNE

# MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Faslu hii inatupasha matokeo ya utafiti wetu pamoja na ufafanuzi wa matokeo hayo kwa njia ya maelezo. Sura hii imegawika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza inatufahamisha kuhusu muktadha ambamo wimbo huu uliimbwa. Ile ya pili inajadili mkabala wa kidini wa kufafanua jazanda za *Wimbo Ulio Bora* huku ya tatu ikijadili mkabala wa kijamii wa kuzifafanua jazanda hizo. Sehemu ya mwisho inadhihirisha jinsi jazanda za kidini za wimbo huu zinavyoweza kutumika katika miktadha ya kijamii.

## 4.2 Muktadha ambamo Wimbo Uliimbwa

Kulingana na Wansbrough (1985:1028), Wayahudi wa kale walikuwa wakiuimba wimbo huu katika sherehe za harusi. Kwa hivyo, asili ya *Wimbo Ulio Bora* inaambatanishwa na sherehe zilizokuwa zikifanyika katika harusi za Wayahudi. Waisraeli, kama jamii zilizowazunguka, sharti walikuwa na sanaa yao ya kimapenzi na katika mazingira yao, lugha ya mapenzi lazima ingetumia mifano na jazanda za kimapenzi kutoka kwa mazingira hayo. Wimbo huu ni kusanyiko la nyimbo kadhaa ambazo zimeunganishwa na maudhui mamoja – mapenzi au upendo. Ulipoimbwa katika sherehe za harusi, wimbo huu ulikusudiwa kufunza watu kuhusu nafasi na haja ya kukuza mapenzi ambayo huwaleta pamoja mwanaume na mwanamke katika ndoa. Ulitukuza mapenzi au upendo kati ya wapendanao na kuiona ndoa kama kilele cha mapenzi yao.

Kusudi la Sulemani kuuimba wimbo huu lilikuwa kuutukuza upendo wa Mungu pamwe na kuashiria upendo wa Mungu kwa Waisraeli kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine, upendo wa Waisraeli kwa Mungu.

Wansbrough (1985:1027) anadai kuwa, upendo wa Mungu kwa Israeli na upendo wa Israeli kwa Mungu unaonyeshwa kwa taswira ya uhusiano kati ya mume na mke.

Kutokana na maoni haya, fasiri yetu ni kwamba, Sulemani anasimamia Mungu ilhali mpenziwe Mshulami anasimamia Israeli. Kwa upande mwingine, Sulemani anasimamia Kristo/Yesu ilhali Mshulami anasimamia kanisa.

Fasiri hii inalingana na maneno yaliyoandikwa katika Isaya 54:5-6 na Yeremia 2:2. Basi, Mungu amechorwa kama mume wa Israeli. Mapenzi yanayoonekana kati ya Sulemani na Mshulami ni kiashiria tu cha mapenzi kati ya Mungu na Israeli.

Wahakiki wa Kikristo wamefuata msimamo wa Wayahudi kuhusu maana ya wimbo huu, ila tu kwao wimbo huu ulikuja kuwa kiashiria cha ndoa kati ya Kristo na kanisa lake au uhusiano kati ya mtu binafsi na Mungu. Madai haya ni kwa mujibu wa Wansbrough (1985:1027) na Baxter (1973:172-178). Tunayaunga mkono maoni haya kwa sababu ya mkabala wa kidini tuliouchukua wa kufasiri jazanda katika wimbo huu.

Kwa hivyo, ni bayana kwamba Sulemani ametumia zaidi jazanda za upendo/mapenzi kuendeleza swala la upendo kati ya Mungu na Israeli na pia kati yake na Mungu. Haiwi ajabu basi tunapomwona Sulemani katika kitabu cha Wafalme wa Kwanza, 6:1-37 akimjengea BWANA (Mungu) nyumba (Hekalu) na kuipamba kwa mapambo ya thamani kubwa kama inavyodhihirika katika Wafalme wa Kwanza, 7:13-51.

**4.3 Mkabala wa Kidini wa Jazanda za *Wimbo Ulio Bora***

Kitabu cha *Wimbo Ulio Bora* kimewekwa katika kitengo cha vitabu vilivyoandikwa kishairi ambavyo Murphey (1989) anaviita "Vitabu vya Hekima)". Vingine ni Ayubu, Zaburi, Mithali na Mhubiri. Akifafanua maana ya Biblia, Murphey (1989:73) amesema kuwa neno hili linamaanisha kitabu kitakatifu au mkusanyiko wa vitabu vilivyokubalika na imani ya Kikristo. Kanisa la Kikristo pia linakubali Biblia kama mwongozo wa imani na tabia kwa wale wanaokiri imani ile. Kwa msingi huu, tulizichanganua jazanda za *Wimbo Ulio Bora* kwa mkabala wa Kidini ambapo tuligundua kwamba kitabu hiki ni wimbo wa mapenzi unaotutaswiria utamu wa uhusiano wa kimapenzi kati ya watu wapendanao kama ishara ya upendo wa Kiungu.

Mfalme Sulemani aliyeandika kitabu hiki aliishi katika enzi ambapo kuabudu sanamu na miungu halikuwa jambo la ajabu. Kwa njia ya kishairi, Sulemani alimtunukia Mungu wake sifa anuwai alizozizua kwa jazanda tofauti tofauti.

Aidha, ilitubainikia kuwa Sulemani alitumia picha ya mpenzi wake na jinsi anavyompenda na kujitoa mhanga ili kuimarisha mapenzi yao. Hii ndiyo ile tuliyoitaja kuwa ishara ya mapenzi ya kiungu; yaani iwapo mtu atampenda binadamu mwenzake kiasi hicho, inapaswa kuwaje kwa Mungu aliye muumba wake? Hili ndilo jambo ambalo mfalme Sulemani analiendeleza katika wimbo huu. Kama kitabu cha kidini, inabainika wazi kuwa Biblia iliandikwa kwa lengo la kuweka msingi na kukuza Ukristo. Kwa sababu hii, katika kufasiri jazanda za *Wimbo Ulio Bora*, tuliupa mkabala wa kidini kipau mbele. Katika kila jazanda, tuligundua kwamba kuna kile kinachozungumziwa lakini kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kutumia vifananishi au mafumbo. Ufuatao ni mjadala wa ufasiri wa jazanda kwa mkabala wa kidini.

(18): Mimi ni mweusi-mweusi, lakini ninao uzuri (1:5a).

Anayezungumza hapa ni binti Mshulami. Anayasema haya baada ya mfalme Sulemani kukubali kumchukua na kumwingiza nyumbani mwake (1:4a). Kitendo hiki kinampa Mshulami furaha kuu kwani inaonekana kwamba alikabiliwa na ushindani mkubwa kama anavyoashiria mwenyewe kwa maneno yafuatayo:

> Kubusu na anibusu kwa kinywa
> chake.
> Maana pambaja zako zapita divai;
> Manukato yako yanukia vizuri;
> Jina lako ni kama marhamu
> iliyomiminwa;
> Kwa hiyo wanawali
> hukupenda. (1:3c).

Pia, katika (1:4e) anasema kuwa:

> "Ndiyo, ina haki wakupende".

Kulikuwa na mabinti wengine wengi waliompenda Sulemani na hata wakatamani awaingize katika vyumba vyake vya kifalme. Mshulami anawaona hawa kama tisho kwa mapenzi yake kwa Sulemani. Katika kujitetea, Mshulami ambaye anashuku urembo wake anasema haitoshi tu kuwa ni mweusi – mweusi, bali anao uzuri. Anamwomba mfalme asimdharau kutokana na weusi-weusi wake lakini atambue uzuri alionao. Anatoa sababu za weusi-weusi ule kama wana wa mamaye ambao walimpa adhabu ya kulinda mashamba yao ya mizabibu ambapo aliunguzwa na jua kali (1:6).

Kwa hivyo, hapo mbeleni alikuwa mrembo zaidi kwani ule weusi - weusi hakuwa nao. Tabia na mienendo yake ambayo ndiyo uzuri anaotaja haijaathiriwa na mazingira ya jua kali alikofanya kazi ya kulinda mizabibu mchana - kutwa. Fasiri tunayoipata hapa ni kwamba mshulami anawakilisha Waisraeli ambao walikabiliana na madhila makuu katika nchi ya utumwa (Misri) na jangwani kwenye safari ngumu ya kwenda nchi ya ahadi (Kanani). Walidhoofika kiafya na maumbo yao yakaumbuka lakini hatimaye walifika salama. Kama Mshulami anavyomsihi mfame asimwache, wana wa Israeli pia wanamwomba Mungu asiwaache kwani bado wangali na moyo wa uzuri; wanampenda sana.

(19): Enyi binti za Yerusalemu (1:5a).

Jazanda mbili zinajitokeza hapa; binti na Yerusalemu. Katika kifungu hiki, binti Mshulami anawaonya wasichana wengine wa mji wa Yerusalemu wasimwangalie kwa jicho la dharau kutokana na weusi-weusi alionao. Anakiri kwamba yeye ni mzuri kama mapazia ya Sulemani. Kwa kawaida, mapambo yanayopatikana katika makasri ya kifalme sharti yawe ni mazuri mno na vivyo hivyo Mshulami ndivyo alivyo mzuri na mrembo.

Mabinti ambao Mshulami anarejelea wanawakilisha wakristo au waokovu. Kulingana na dini ya Kikristo, waokovu ni watu walioteuliwa na kupendwa na Mungu. Wanaporejelewa kama 'mabinti', inadhihirisha upendo uliopo kati ya Mungu na waokovu kwa kulinganishwa na uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke wanaotarajia kufunga ndoa. Kwingineko ambako mabinti wametajwa katika wimbo huu ni 1:3, 1:4, 1:5, 1:6, 3:10, 6:9 na 8:4. Vifungu hivi vyote vinaendeleza swala la uhusiano kati ya wapenzi kama kiashiria cha uhusiano wa upendo kati ya Mungu na wakristo. Waumini hawa wa dini ya Kikristo huitumia Biblia kama mwongozo na kipimio cha imani yao.

Yerusalemu ulikuwa ni mji wa jamii ya Wayebusi kabla ya mfalme Daudi na jeshi lake kupigana nao na kuuteka mji huo. Haya ni kulingana na kitabu cha Samweli wa Pili 5:6-10. Baada ya Daudi kupiga ngome ya Sayuni, alikaa ndani yake na akaiita Mji wa Daudi. Ni katika mji huu ambako Sulemani, (mwanawe Daudi) alijenga hekalu la kuabudia Mungu.

Katika hekalu hiyo, sanduku la agano liliwekwa. Jambo hili liliufanya mji huu kuwa maarufu sana kati ya Wayahudi. Kuna majina mengine pia ambayo yanatumiwa katika Biblia kurejelea Yerusalemu; haya ni pamoja na:

- Mji mtakatifu (Nehemia 11:1, Isaiya 1:26; Ufunuo wa Yohana 21: 29)
- Mahali pa wokovu (Isaya 4:3; Luka 2:38)
- Makazi ya Mungu (Kutoka 25:8; Jeremia 3:17)
- Yerusalem mpya (Ufunuo wa Yohana 21:26)
- Maskani ya Mungu (Ufunuo wa Yohana 21:3)
- Mji wa Mungu (Zaburi 87:3)
- Arieli (Isaya 29:1)
- Mji wa Daudi (2 Samweli 6:12)
- Mji wa Mfalme mkuu (Mathayo 5:35)
- Mji wa Bwana (Isaya 60:14)
- Mji wa Bwana wa majeshi (Zaburi 48:8)
- Mji wa kweli (Zekaria 8:3)
- Ukamilifu wa uzuri (Maombolezo 2:15)
- Furaha ya dunia yote (Maombolezo 2:15)
- BWANA yupo hapo (Ezekieli 48:35)
- BWANA ni haki yetu (Yeremia 23:6; 33:16)
- Salemu (Mwanzo 14:18).

Murphey (1989:193).

Kama inavyoonekana, majina haya yote yanadhihirisha kwamba Yerusalemu ni mji unaoambatanishwa na utukufu wa Mungu. Kulingana na mafundisho ya Ukristo, Yerusalemu hufananishwa na mbinguni ambayo ndiyo makao ya Mungu, yaani Yerusalemu mpya. Ufunuo wa Yohana 21:1-8 unazungumza kuhusu Yerusalemu mpya ambao ndio ufunuo alioonyeshwa Yohana kama inavyodhihirika katika nukuu ifuatayo:

> [1] Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena. [2] Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.

> [3] Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi
> ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na
> wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao,
> nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe
> atakuwa pamoja nao. [4] Naye atafuta kila chozi katika
> macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala
> maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo
> tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.
> [5] Na yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema,
> Tazama, nayafanya yote kuwa mapya. Akaniambia,
> Andika ya kwamba maneno hayo ni amina na kweli.
> [6] Akaniambia, Imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega,
> Mwanzo na Mwisho. Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya
> chemchemi ya maji ya uzima, bure. [7] Yeye ashindaye
> atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye
> atakuwa mwanangu. [8] Bali waoga, na wasioamini, na
> wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi,
> na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao
> ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo
> mauti ya pili.

Basi, Mshulami anaposema katika *Wimbo Ulio Bora* 1:5b kwamba, " Enyi binti za Yerusalemu", anamaanisha wale watu wote watakaofuzu, kulingana na masharti yaliyowekwa katika Ufunuo wa Yohana 21:7-8, kuingia katika mji ule mtakatifu; Yerusalemu mpya yaani Mbinguni ambako kumeandaliwa watu walio waokovu. Mji huu mtakatifu; Yerusalemu," anamaanisha wale wote watakaofuzu, kulingana na masharti yaliyotajwa katika ufunuo wa yohana 21:7-8, kuingia katika mji ule mtakatifu; Yerusalemu mpya yaani mbinguni ambako kumeandaliwa watu walio waokovu. Mji huu mtakatifu (Yerusalemu mpya), wasemekana kuwa umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Ujenzi na mapambo ya mji ule mtakatifu (Yerusalemu mpya) yameelezewa kwa sifa za kuvutia kwelikweli katika Ufunuo wa Yohana 21:17-27. Kwa mfano mistari ya 18 na 19 yasema hivi:

> "Na majenzi ya ule ukuta wake yalikuwa ya yaspi, na mji ule ulikuwa wa dhahabu safi, mfano wa kioo safi. Na misingi ya ukuta wa mji ilikuwa imepambwa kwa vito vya thamani vya kila namna."

Ujenzi na mapambo ya thamani kubwa jinsi hii ndivyo baadhi ya vitu ambavyo huwapa waumini wa dini ya Kikristo shime na motisha kwendelea kuishi maisha 'matakatifu' ambayo hayatawafanya wachujwe na kuikosa raha ya mji ule. Msitari unaoweka masharti wazi na hivyo kuwa changamoto kwa waumini wa Kikristo ni wa 27 katika ufunuo 21 unaosema kwamba:

"Na ndani yake hakitaingia kamwe chochote kilicho
kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo,
bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha
Mwana - Kondoo".

(20): Jua limeniunguza (1:6a)

Kwa kawaida, jua linapowaka sana husababisha ongezeko la joto. Miale ya jua yenye joto inapomulika kitu kwa muda mrefu, kitu hicho huungua na aghalabu hubadilika rangi. Rangi yake asilia hufifia, kikabaki kimechujuka. Kutokana na hali hii ya kuchujuka rangi, kitu hicho huwa hakivutii tena kama hapo mbeleni. Vilevile, thamani yake hushuka na iwapo ni kifaa cha kupigwa bei, gharama yake huenda chini kwa sababu ubora wake umefifia na hakipendezi kama hapo awali. Hii ndiyo hali ambayo Mshulami anajikuta kwayo.

Katika *Wimbo Ulio Bora* 1:5, Mshulami anasema:

"Mimi ni mweusi-mweusi. lakini
ninao uzuri,
Enyi binti za Yerusalemu,
Mfano wa hema za Kedari,
Kama mapazia yake Sulemani."

Anayarudia maneno haya katika 1:6 kwa sababu hapendezwi na hali iliyomfika ya weusi - weusi. Akiwa katika hali ya masikitiko anasema:

" Msinichunguze kwa kuwa ni
mweusi – mweusi,
Kwa sababu jua limeniunguza".

Ndugu zake binti Mshulami walijaribu kuupinga uhusiano wake wa kimapenzi na Sulemani kwa vile walimwona bado mdogo wa umri. Maneno yafuatayo yanadhihirisha msimamo wao wanaposema:

"Kwetu sisi tuna umbu mdogo,
Wala hana maziwa;
Tumfanyieje umbu letu,
Siku atakapoposwa?"
(*Wimbo Ulio Bora* 8:8).

Kwa vile hawakufurahia uhusiano ule, labda kwa kuogopa kwamba Sulemani angempotezea muda dada yao, ndugu zake Mshulami walitamani awe ukuta ili wamjengee buruji za fedha au awe mlango wamhifadhi kwa mbao za mierezi. Ndugu hawa waonekana kuwa waliogopa dada yao asijiingize katika mapenzi akiwa mdogo; walielewa madhara yake. Hata hivyo, msichana mwenyewe hakusikia bali aliwajibu katika *Wimbo Ulio Bora* 8:10 kuwa yeye si mtoto tena kwa maneno haya:

> "Mimi nalikuwa ukuta,
> Na maziwa yangu kama minara;
> Ndipo nikawa machoni pake
> Kama mtu aliyeipata amani.

Walipogundua kwamba dada yao habadili msimamo wake kuhusu mapenzi yake kwa Sulemani, ndugu hao walikasirika sana na wakaamua kumchukulia hatua kali. Ili kumkosesha nafasi ya kuonana na Sulemani, walimpa kazi ya kulinda mashamba yao ya mizabibu. Hii ilikuwa adhabu kwani ni kazi iliyochukua wakati wake wote. Aliifanya kazi hiyo juani na kwa hivyo jua likamchoma sana, likamwunguza hadi akachujuka na mwishowe akawa mweusi-mweusi. Urembo wake ulififia kweli.

Tunalifananisha jua hili lililoiunguza ngozi iliyokuwa nzuri hapo mbeleni ikawa baya na mateso ambayo yaliwakumba Waisraeli tangu utumwani Misri, njaa na kiu jangwani na mwishowe vita vya kuiteka miji ya Kanani. Kama ambavyo Mshulami hakukatishwa tamaa na upinzani wa ndugu zake dhidi ya upendo wake kwa Sulemani, ndivyo Israeli hawakutamaushwa na dhiki walizokabiliana nazo. Mwishowe walifika mji wa ahadi kama inavyodhihirika katika Yoshua 11:21-23:

> "…Basi Yoshua akaitwaa hiyo nchi yote, sawasawa na hayo yote, BWANA aliyokuwa amemwambia Musa; Yoshua naye akawapa Israeli kuwa ni urithi wao, sawasawa na walivyogawanyikana kwa kabila zao. Kisha nchi ikatulia isiwe na vita tena".

Kulingana na Ukristo, waokovu watakaovumilia mpaka mwisho ndio watakaourithi uzima wa milele. Hawa waumini wanamithilishwa na Waisraeli ambao waling'ang'ana kwa zaidi ya miaka arubaini. Vivyo hivyo, licha ya Mshulami kupingwa na ndugu zake na kuadhibiwa juani kama mlinzi wa mashamba ya mizabibu, bado aliendeleza uhusiano wake na Sulemani na mwishowe akafanikiwa kuolewa naye.

(21): Wana wa mamangu (1: 6b)

Kijuu juu, kama tulivyokwishaelezea katika mfano wa (20), " wana wa mamangu" ni jazanda inayorejelea ndugu zake Mshulami. Mshulami aliyasema maneno haya kumaanisha ndugu zake ambao waliupinga sana uhusiano/mapenzi kati ya dada yao na Sulemani. Kifasiri, wana ni wapinzani au maadui wa imani ya waokovu ambao hujaribu kuingilia na kupinga upendo wa waumini kwa Kristo. Tunafahamu kwamba mambo kama haya hutokea katika ulimwengu wa sasa ambapo watu wa familia hupinga imani ya kidini ya mwenzio huku wakitaka aidha afuate dini wanayoifuata wao au nyingine tofauti na anayoifuata au katu asifuate yoyote ile. Hii ndiyo sababu serikali nyingi zimeingilia jambo hili na kuzua swala la "uhuru wa ibada" katika katiba zao kama ilivyo katika nchi ya Kenya. Hali hii inawapa wananchi uhuru wa kuamua ni dini ipi waifuate mradi tu haitishi usalama wa wengine.

(22): Mlinzi wa mashamba ya mizabibu (1: 6c)

Tunaambiwa kwamba wana wa mamake Mshulami walimkasirikia kwa sababu ya kujiingiza katika mapenzi angali mdogo. Walipinga sana uhusiano huo kati ya dada yao na Sulemani. Ili kumkosesha nafasi ya kuonana na mpendwa wake Sulemani, walitumia mbinu ya kumfunga shambani ambapo walimweka awe mlinzi wa mashamba ya mizabibu. Mashamba hayo ya mizabibu yalikabiliwa na hatari ya kuharibiwa na mbweha kama inavyotajwa katika *Wimbo Ulio Bora* 2:15. 'Shamba la mizabibu' ni kifungu ambacho kimetumiwa kijazanda kumaanisha maisha ya Kikristo ambayo yanafaa kuonyesha matokeo (matunda) mazuri yanayolingana na imani ya dini hiyo. Basi, zabibu zinalinganishwa na matendo mema ambayo ni matunda ya imani. Kuhusiana na haya, Biblia inasema katika Yakobo 2:17 kwamba 'imani isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake'.

Kifasiri, ulinzi wa mashamba ya mizabibu ni hali inayofananishwa na watu wanaojiingiza na kushiriki katika mambo ya kiumma huku wakiyasahau mambo yao ya kindani. Mambo ya kibinafsi kama vile familia yanafaa kutangulia yale ya umma. Kwa hivyo, kifungu hiki ni onyo kwa watu ambao huenda washiriki sana maswala ya umma kisha wakayasahau yale ya kibinafsi.

Kuhusiana na imani ya kidini, kifungu hiki kinatoa funzo au onyo kwa waumini wa Kikristo, wachungaji, wainjilisti au hata wazee wa kanisa kwamba wanapofanya kazi ya kuwalea wengine kiimani, wakumbuke kwamba wao ndio wanaostahili kuimarika kiroho zaidi ili waweze kuwalea wengine. Watu kama hawa husahau kuomba na kusoma neno la Mwenyezi Mungu. Aidha, wao hukosa nafasi ya kuishi na kuzungumza na familia zao. Hii ni hali hatari na ndio sababu Mshulami anasema katika *Wimbo Ulio Bora* 8:12 kwamba:

> " Shamba langu la mizabibu. lililo
> langu mimi, li mbele yangu".

Kifungu hiki kinamaanisha kwamba pana haja ya kuweka mbele maswala ya kibinafsi. Madhara ya kujisahau huku mtu akishiriki katika umma yanadhihirishwa na binti Mshulami katika *Wimbo Ulio Bora* 1:6 anapolalamika kwa maneno yafuatayo:

> " Msinichunguze kwa kuwa ni
> mweusi-mweusi,
> Kwa sababu jua limeniunguza.
> Wana wa mamangu
> walinikasirikia.
> Waliniweka niwe mlinzi wa
> mashamba ya mizabibu;
> Bali shamba langu mwenyewe
> sikulilinda".
> (1:6)

(23): Ua la uwandani (2:1a).

Ua ni sehemu ya mmea inayochanua na aghalabu ndiyo sehemu ya uzazi ya mmea. Kwa jumla, ua huashiria mapenzi, upendo au kupendwa na mtu anapopewa ua na mpenzi wake huonyesha jinsi anavyompenda. Takriban maua yote hunukia vizuri pamoja na kuwa na rangi inayopendeza; sifa ambazo huyafanya maua yapendwe na watu wengi. Kulingana na hatua za upambanuzi za Leech (1969), tuligundua mambo yafuatayo kutoka kwa jazanda hii. Maana ya juu ya ua la uwandani (mahali tambarare) ni ule uwezo wa kuvutia macho kwani huwa limesimama peke yake, huonekana bila pingamizi yoyote hata kutoka mbali kwa sababu uwandani hakuna miti wala miinuko. Kitu kizuri huvutia macho. Maana ya ndani ni jinsi Sulemani anavyomfananisha Mungu wake na ua.

Kama ambavyo ua hupendwa, ndivyo Sulemani anavyompenda Mungu na vivyo hivyo Mungu anawapenda Waisreali. Kizungumzwa ni Mungu ilhali kifananishi ni ua la uwandani. Kiungo ni upendo wa Sulemani kwa Mungu na upendo wa Israeli kwa Mungu na kwa upande mwingine, upendo wa Mungu kwa Sulemani na Israeli.

Kulingana na vipengele vya Pragmatiki ya Grice (1967), katika jazanda hii tuligundua kwamba Kaida ya Ushirikiano imevunjwa. Hii ni kwa sababu kanuni ya "namna" ambayo inashauri upunguzaji wa utata katika mawasiliano, haijatiliwa maanani lakini badala yake imepuuzwa. Katika kiambatisho chetu, haieleweki wazi iwapo nafsi "mimi" inarejelea Sulemani au mpenzi wake kwani hata hatwambiwi anayezungumza ni nani. Hali hii inasababisha utata mwingi wa kimaana. Hata hivyo, ufasiri wetu umeweka mambo haya bayana.

(24): Nyinyoro ya mabondeni (2:1b).

Nyinyoro ni aina ya mmea wenye shina kama la kitunguu na unaotoa maua mekundu. Kwa upande mwingine, mabonde ni sehemu za ardhi zilizo baina ya vilima viwili na aghalabu hupitiwa na mito. Sifa kuu ya mabonde ni kuweko kwa unyevu mwingi katika misimu yote ikilinganishwa na sehemu zilizopazunguka mahali pale.

Maana ya juu ya jazanda hii ni kwamba, mmea huu unapokua bondeni, hauwezi kukauka kwa sababu bondeni kuna unyevu kwa misimu yote. Kwa hivyo, nyinyoro hii itatoa maua wakati wake ukifika. Vilevile katika bonde, huwa kuna rutuba kwa sababu mchanga wa kutoka sehemu za miinuko hukwamilia pale. Bila shaka, ua la bondeni litakua likiwa na afya na hivyo litavutia macho. Anayezungumza hapa anajifananisha na nyinyoro ya mabodeni yenye afya kinyume na mimea inayokua sehemu kavu. Mzungumzaji ambaye ni Mshulami, anajitwika sifa kwa nia ya kumvutia mpenzi wake (Sulemani).

Maana ya ndani ya jazanda hii tunaiambatanisha na Sulemani. Sulemani anamuona Mungu wake kama ule mmea ambao haunyauki kwa kukua bondeni penye unyevu na rutuba siku zote. Anamtwika sifa Mungu wake kwamba wema na fadhila zake hazipungui kamwe siku zote.

Mungu ni wa kutegemewa wakati wote kwani uwezo wake wa kutenda mambo makuu haupungui. Hii ndiyo sababu Wakristo wanafuata mafundisho kwamba "Mungu ni yule yule jana, leo na milele; habadiliki." Kama vile nyinyoro ya mabondeni huendelea kukua misimu yote, vivyo hivyo Mungu huendelea kujidhihirisha wakati wote kwani hawekewi mipaka ya nyakati; uungu wake haufifii daima.

(25): Hua wangu, mafichoni mwa
jabali,
Katika sitara za magenge,
Nitazame uso wako, nisikie sauti
yako
Maana sauti yako ni tamu na
uso wako mzuri.
(2:14).

Hua ni aina ya ndege wa jamii ya njiwa. Ndege huyu anahusishwa na sifa za upole na kutokuwa na madhara yoyote. Ndege huyu si hatari kwa vyovyote vile. Mara nyingi, ndege huyu huchukuliwa kuashiria amani.

Maana ya juu ni kwamba sulemani anamsifu mpenzi wake kwa kumtwika sifa za upole, amani na utulivu. Hii ndio sababu sulemani anasikika akimshawishi mpenzi huyo kwamba japo amejifungia kwenye vyumba vya juu (mafichoni mwa jabali, katika sitara za magenge), angependa kutazama uso wake na kuisikia sauti yake. Kwa hivyo, anamwomba ajitokeze ili amuone na amsikie kwa kuwa sauti yake ni tamu na uso wake ni mzuri (wavutia).

Maana ya ndani - Sulemani anamlinganisha Mungu wake na hua. Kwa Sulemani, Mungu wake ni mpole, mtulivu, mwenye amani na asiye hatari. Anaomba kumuona Mungu (kuwa na ushirika naye) kumaanisha jinsi anavyompenda kwa kudai kwamba sauti yake ni tamu na uso wake mzuri. Sulemani angependa kuongea na Mungu na hata kumuona kwa uso. Hali hii inaonyesha ushirikiano wa karibu sana uliokuweko kati ya Sulemani, Israeli na Mungu. Kizungumzwa ni Mungu ilhali kifananishi ni hua. Kiungo ni sifa za hua; upole, utulivu na amani ambazo zinahamishwa kwa Mungu. Kanuni ya 'namna' katika Kaida ya Ushirikiano imevunjwa.

Hii ni kwa sababu, kumlinganisha Mungu na hua anayejificha katika jabali, na sitara za magenge, ni hali inayotatanisha sana. Mungu hajifichi. Aidha, Sulemani anasihi Mungu atokee ili auone uso wake na kusikia sauti yake. Ni Vigumu kumwona Mungu uso kwa uso na kwa hivyo haibainiki wazi Sulemani anamaanisha nini. Vilevile, inaaminika kuwa wakati mwingine Mungu hufanya matendo ya hatari tofauti na alivyo hua asiye madhara.

(26): Tukamatie mbweha,
Wale mbweha wadogo,
Waiharibuo mizabibu,
Maana mizabibu yetu
Yachanua.
(2:15).

Mbweha ni mnyama mwenye umbo la mbwa na huishi msituni. Yeye ni mbwa mwitu na mla nyama. Kulingana na utamaduni wa Kiebrania, mbweha wanafananishwa na adui. Ni wanyama ambao huharibu mimea hasa wanapoyafanya mashamba kuwa makazi yao. Kwa mfano, huwa wanaangusha zabibu wanapofanya mizabibu kuwa maficho yao.

Maana ya juu - Wapenzi hawa wanaomba shamba lao la mizabibu lilindwe dhidi ya uharibifu wa wale mbweha wadogo wanaoiharibu mizabibu ambayo inachanua. Aidha, wanamaanisha kwamba mapenzi yao ambayo yanaendelea kushamiri kama mizabibu inayochanua, yanaingiliwa na maadui (mbweha). Wanaomba kuondolewa kwa maadui ili mapenzi yao yasiharibiwe. Ndugu zake Mshulami ambao walipinga uhusiano kati ya dada yao na Sulemani ndio wanaolinganishwa na mbweha wanaoharibu mizabibu inayochanua. Mizabibu ni mapenzi kati ya Sulemani na binti Mshulami.

Maana ya ndani - Sulemani ni mcha Mungu. Mbweha ni maovu na vishawishi ambayo vingeweza kutinga na kuathiri imani yake kwa Mungu. Imani ya Sulemani ambayo imefikia kiwango cha juu, inakabiliwa na hatari ya kufifishwa na maovu yanayomkabili katika maisha ya kila siku. Sulemani aliishi katika enzi ambapo jamii nyingi ziliabudu miungu na sanamu. Kwa hivyo, wale mbweha wadogo ni jazanda inayorejelea mambo madogomadogo ambayo yanaweza kutinga imani ya waumini na kulegeza msimamo wao katika dini na imani kwa Mungu wao.

Kizungumzwa ni maovu na vishawishi ilhali kifananishi ni mbweha. Kiungo ni uharibifu wa mbweha unaofananishwa na athari za maovu kwa imani katika Mungu.

(27): Bustani iliyofungwa ni umbu
langu, bibi arusi,
(4:12a).

Katika jazanda hii, maana ya juu tunayoipata ni kwamba Sulemani ana bustani yake iliyopandwa maua na miti na yeye tu ndiye ana kibali cha kuistarehe. Wapita njia wanaonywa dhidi ya kuingia kwenye bustani hiyo. Anatoa onyo kwamba mpenzi wake (Mshulami) asitongozwe na mwanaume yeyote yule.

Maana ya ndani ya jazanda hii ni kwamba bustani ni Mungu wake Sulemani na anaposema kuwa ameifunga, kidokezo tunachopata ni kwamba anampenda Mungu wake na hata kummiliki kabisa hivi kwamba anambinafsisha. Kizungumzwa ni Mungu. Kifananishi ni bustani iliyofungwa ilhali kiungo ni kupenda kitu hadi kukichukulia kama kitu cha kibinafsi. Sulemani anamchukulia Mungu kama mali ya kibinafsi. Kaida ya Ushirikiano imeasiwa kwa sababu kanuni za "namna" na "thamani" zimevunjwa kutokana na Sulemani kumchukulia umbu yake (dadake) kuwa mpenzi wake. Si kawaida mwanaume kumtongoza dada yake. Uhusiano wa aina hii ni haramu kulingana na imani ya Kikristo. Jazanda hii imetumiwa kutilia mkazo uhusiano kati ya Sulemani na Mungu kwa kuulinganisha na uhusiano kati ya mtu na umbu au ndugu yake ambao kutokana na heshima huepuka kukoseana.

(28): Kijito Kilichofungwa. (4:12b).

(29): Chemchemi iliyotiwa muhuri. (4:12c).

Jazanda hizi mbili zina maana za juu na za ndani sawasawa na maana za jazanda iliyozitangulia ya mfano wa (27). Katika jazanda ya (28), kizungumzwa ni Mungu ilhali kifananishi ni kijito kilichofungwa. Katika jazanda ya (29), kizungumzwa kinabakia kuwa Mwenyezi Mungu ambaye anafananishwa na chemchemi iliyotiwa muhuri. Katika jazanda zote mbili, kiungo ni kimoja, ile hali ya Sulemani kummiliki Mungu kama kitu cha kibinafsi.

Katika jazanda ya kijito kilichofungwa, kanuni iliyokiukwa katika Kaida ya Ushirikiano ni ya "namna" kwa sababu Mungu si kijito. Pia, kufunga kijito kinachotiririka ili kisitumiwe na watu wengine hata majirani, si jambo la kawaida. Kijito huwa mali ya umma na hutumiwa na watu wengi bali si kitu cha mtu binafsi. Katika jazanda ya chemchemi iliyotiwa muhuri (mfano wa 29)), utata unazuka pale ambapo haibainiki vile chemchemi itatiwa muhuri. Aidha, utata unatokea katika kujaribu kubaini nia ya kutiwa chemchemi muhuri ilhali chemchemi inafaa kutumiwa na watu wote. Hata hivyo, tumebaini kuwa wazo kuu linalojitokeza katika jazanda hizi ni umilikaji unaotokana na hali ya kukipenda kitu sana hadi kufikia kiwango cha kukibinafsisha hata ingawa ni mali ya umma.

(30): Machipuko yako ni bustani ya
komamanga,
Yenye matunda mazuri, ...
(4:13).

Komamanga ni aina ya tunda. Katika jazanda hii, Sulemani anaendelea kumsifu mpenzi wake kwa maneno yenye kuvutia. Anamfananisha na bustani ya komamanga, bustani ambayo huzaa matunda mazuri. Basi, matunda haya yanalika kutokana na uzuri wake. Yana ladha nzuri. Ni matunda matamu la sivyo Sulemani hangesema kuwa ni matunda mazuri

Maana ya juu ya jazanda hizi ni kwamba maneno na tabia za mpenzi wa Sulemani ni kama matunda mazuri. Ni tabia zisizochukiza bali zinapendeza. Aidha, Sulemani anausifu urembo wa mpenzi wake ambao unaongezewa uzuri na umri mdogo alionao msichana huyo. Mambo yote yanayohusiana na mpenzi wake ni mazuri. Hii ni njia nyingine ya kusema kwamba, mpenzi wake hachukizi kwa hali yoyote ile.

Katika maana ya ndani, Sulemani anadhihirisha anavyompenda Mungu kwa dhati kupitia jazanda hii. Mawazo na matendo ya Mungu ni mema. Mungu hachukizi na hii ndiyo sababu Sulemani anayalinganisha matendo au mawazo ya Mungu na bustani ya komamanga, yenye matunda mazuri, maua na miti aina nyingi yenye kunukia vizuri. Hapa Sulemani anaiendeleza sifa moja kuu ya Mungu ambayo ni wema; Mungu ni mwema.

Kizungumzwa ni matendo ya Mungu yanayofananishwa na bustani ya komamanga, bustani yenye matunda mazuri, maua na miti tofauti tofauti inayopendeza. Kiungo ni ile hali ya kuvutia. Bustani ya komamanga inapendeza kutokana na matunda mazuri, maua na miti aina tofauti. Kwa jinsi hiyo, matendo mazuri ya Mungu yanampendeza sana Sulemani, kwa hiyo anampenda sana.

(31): Kisima cha maji yaliyo hai. (4:15).

Kulingana na mafundisho ya Kikristo ambayo ndiyo msingi wa uchambuzi wetu, maji yaliyo hai ni amani na utoshelevu zipatikanazo baada ya mtu kukiri imani katika Mungu/Yesu na kukubali imani hiyo imwongoze katika maamuzi yake. Wakristo wanaamini kwa dhati kuwa mtu akiyanywa maji hayo haoni kiu tena; yaani anakuwa kiumbe kipya kwa sababu ya kuyaacha maisha maovu ya kale. Hiyo hali ya kuweza kukoma kufanya mambo ambayo mtu aliyazoea hapo mbeleni ni kama kukata kiu kwa kuyanywa maji. Tofauti iliyoko kati ya maji ya kawaida na maji ya Kibiblia ni kwamba anayeyanywa haya ya Kibiblia anapata mabadiliko katika mtindo wake wa maisha. Walioyanywa maji yaliyo hai inasemekana kuwa "wameokoka' na aghalabu hawatendi matendo ambayo yanaaminika kuwa ni kinyume cha mafunzo ya Biblia. Maji ya kawaida hayana sifa hii ya kuweza kukatisha kiu kabisa kwani haja ya kuyanywa humrudia mtu mara kwa mara.

Maana ya juu ya jazanda hii ni kwamba, Sulemani anamuona mpenzi wake kama kisima kisichokauka maji. Pia, furaha anayoonyeshwa na mpenzi huyo humfanya apate amani na utulivu moyoni mwake kila wakati. Maana ya ndani ni tumaini la Sulemani katika Mungu wake. Wema wa Mungu hauishi na kwa hivyo Sulemani anapata nguvu kuendelea kumtumaini. Kwa kumwamini na kumtumaini Mungu, Sulemani anapata utulivu na amani moyoni kama mtu aliyekunywa maji baridi ya kisima na kukata kiu.

Kizungumzwa ni Mungu ilhali kifananishi ni kisima cha maji yaliyo hai. Kiungo ni kutotamauka kwa yule anayemtumaini Mungu kama ilivyo kisima kisichokauka daima. Kanuni ya "namna" imekiukwa kwani dhana ya "maji yaliyo hai" ni ngumu kuielewa na kuifafanua. Kitu kilicho hai, sharti kife. Je, maji haya yanayosemekana kuwa yako hai yatakufa? Hili ni swala ngumu na linazua utata wa kimaana.

Maana tunayoipata katika jazanda hii ni kwamba mtu yeyote anayeupokea wokovu, maisha yake hayatakomea kaburini baada ya kifo, bali ataishi tena katika hali ya kiroho huko Yerusalemu mpya; yaani mbinguni.

(32): Wako malkia sitini, na masuri themanini,
Na wanawali wasiohesabika;
Hua wangu, mkamilifu wangu, ni mmoja tu,
Moto wa pekee wa mamaye.
(6:8-9).

Katika kifungu hiki, jazanda tatu zinajitokeza wazi. Hizi ni:

- Malkia sitini
- Masuria themanini
- Wanawali wasiohesabika

Kutokana na jazanda hizi, tunakisia kwamba zinarejelea wanawake ambao Sulemani alikuwa na miadi nao. Wengine walikuwa bibi zake (malkia 60) ilhali wengine si bibi zake bali ni wanawake wa kando. Katika kitabu cha Wafalme wa Kwanza, 11:3, tunajulishwa kuwa mfalme Sulemani alikuwa na mabibi 700 na masuria 300. Sulemani anakiri kuwa wanawake hawa wako na anawapenda wote, lakini anayempenda zaidi ni huyu Mshulami kwani yeye tu ndiye aliye mkamilifu; (*Wimbo Ulio Bora* 6:9). Anasemwa kuwa yeye ni mzuri katika wanawake; amewashinda wanawake hao wengine wote kwa urembo na uzuri (6:1b).

Maana ya ndani ni kwamba, jazanda hizi tatu zinarejelea miungu ambayo inanaweza kuabudiwa badala ya Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, Sulemani anakiri kuwa hua wake (Mungu) aliye mkamilifu, ni mmoja tu. Basi, Sulemani anamlinganisha Mungu na binti mrembo (mkamilifu na mtoto we pekee wa mamaye) ambaye hamna mwingine mithili yake. Hali hii inadhihirisha mapenzi aliyonayo Sulemani kwa Mungu wake. Hata hivyo, mambo mawili yanakanganya katika jazanda hii kwa sababu ya kuvunjwa kwa kanuni ya "nanma" katika Kaida ya Ushirikiano kuambatana na Pragmatiki ya Grice (1967):

i) Haieleweki iwapo Sulemani anaongea ukweli au uongo anapokiri mapenzi yake kwa mwanamke mmoja tu ilhali ako na wengine wengi hata asiojua idadi yao (wasiohesabika).

ii) Inatatanisha kwamba kati ya wanawake wengi alionao Sulemani, mmoja tu ndiye aliye mkamilifu. Je, ukamilifu huu ni upi na mipaka yake ni ipi? Wanawake wengine walikosa nini?

Kulingana na uchambuzi wetu, Sulemani hangemlinganisha Mungu wake na chochotekile; si miungu wala sanamu. Alimfanyia Sulemani mambo mengi kama vile kumpa hekima nyingi, sifa kuu na mali nyingi. Hii ndiyo sababu anakiri mapenzi yake kwa Mungu huyu na hawezi kumfananisha na miungu wala sanamu yoyote ile.

(33): Mwako wake ni mwako wa moto. (8:6e).
Katika jazanda hii, mapenzi yanafananishwa na moto; kwamba mapenzi huwaka kama moto uwakavyo. Moto huunguza chochote kilicho karibu hadi kikawa majivu. Msichana (Mshulami) anakiri nguvu za mapenzi ya mpenzi wake Sulemani hivi kwamba hawezi kukaa mbali naye. Hii ndiyo sababu katika 8:6a-c anasema:

"Nitie kama muhuri moyoni mwako,
Kama muhuri juu ya mkono
wako;
Kwa maana upendo una nguvu
kama mauti.
Na wivu ni mkali kama ahera".

Binti huyu anasema upendo una nguvu kama mauti. Hii ni kusema kwamba kifo hakiwezi kuzuiliwa kabisa; kikija hakizimiki. Vilevile, mapenzi hayawezi kuzimwa. Msichana huyu, kwa kuzidiwa na upendo, anamwomba Sulemani amtie kama muhuri moyoni mwake. Maana ya ndani tunaipata tunapohamisha mawazo ya Mshulami kuhusu upendo hadi kwa Sulemani na jinsi anavyompenda na kum'enzi Mungu wake. Sulemani anasema katika *Wimbo Ulio Bora* 8:7 kwamba maji mengi hayawezi kuuzimisha upendo, wala mito haiwezi kuuzamisha. Maneno haya yanadhihirisha jinsi Sulemani kama mcha Mungu alivyompenda Mungu wake. Hakuna kitu au jambo lolote ambalo lingeweza kudidimiza upendo wake kwa Mungu.

Katika hali ya kawaida, tunafahamu kuwa moto huzimwa kwa kutumia maji. Kinyume chake, Sulemani anadai kwamba, maji na mito haziwezi kuuzima upendo wake kwa Mungu. Upendo kama huu umetajwa katika Warumi 8:35 palipoandikwa kwamba:

> "Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo?
> Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi,
> au hatari, au upanga?"

Wakristo walioshika dini kwa mazingatio makuu huamini na kukiri kwamba hakuna kitu kinachoweza kuwatenganisha na upendo wa Mungu.

Kizungumzwa ni mapenzi ya Sulemani kwa Mungu ilhali kifananishi ni mapenzi ya Mshulami kwa Sulemani. Kiungo ni nguvu za mapenzi ambazo haziwezi kuzuilika kamwe. Kanuni ya "namna" inavunjwa katika jazanda hii pale ambapo Mshulami anasema kuwa maji mengi hayawezi kuuzimisha wala mito kuuzamisha upendo. Utata unazuka hapa kwa sababu tunaelewa kwamba hata wazima moto aghalabu hutumia maji kuuzima moto. Je, moto huu ni upi usiozimika kwa kutumia maji mengi hata kiasi cha mito? Tunaelewa kwamba nia ya Sulemani ni kusisitiza upendo wake kwa Mungu hivi kwamba hakuna kitu chochote kinanaweza kumtoa katika imani ya Mungu. Hii si imani haba!

(34): Na miali yake ni miali ya
Yahu.
(8:6f).

Miali ya moto wa Mungu ni mikali mno; inatoka katika ziwa la moto kama ilivyotajwa katika Ufunuo wa Yohana 19:20, 20:10 na 21:8. Miali ya mapenzi ya binti Mshulami kwa Sulemani ni mikali mno kwani katika mfano wa (33), inasemekana kuwa inatoa mwako wa moto. Upendo wa Sulemani kwa Mungu wake unafananishwa na ukali wa miali ya ziwa la moto. Maelezo haya yanadhihirisha jinsi Sulemani anavyompenda Mungu na katika msitari unaofuata wa (8:7), yasemekana kuwa maji mengi hayawezi kuuzimisha upendo, wala mito haiwezi kuuzamisha. Maji na mito hapa zimetumika kijazanda kuashiria kwamba hakuna jambo lolote lile ambalo linanaweza kumshawishi Sulemani dhidi ya kumsujudu Mungu wake.

(35): Mimi nalikuwa ukuta,
Na maziwa yangu kama minara;
Ndipo nikawa machoni pake
Kama mtu aliyeipata amani.
(8:10).

Kutokana na kifungu hiki, fasiri zifuatazo zinajitokeza:

i) Mshulami ambaye anatajwa kwa kirejeleo "mimi" alikuwa ukuta; posa yake ilipingwa sana na kaka zake (8:8a) hadi ikawa kwamba hafikiki na wanaume waliomtamani. Maombi yote ya ndoa aliyopewa, aliyakatalia mbali. Hii ndiyo maana alionekana kuwa ukuta kwa vile ilikuwa vingumu sana kwake kuchumbiwa. Inaonekana kwamba kaka zake walimwekea vikwazo vikali kwa vile walimwona bado akiwa mdogo asiyefikisha umri wa ndoa, (8:8a). Hata hivyo, binti mwenyewe anaasi matarajio ya kaka zake anapokiri kwamba yeye si mtoto tena bali amebaleghe na tayari amepata chaguo lake la moyo - Sulemani.

ii) Maana ya ndani ya kifungu hiki inarejelea uhusiano kati ya Mungu na taifa la Israeli. Mungu akichukua mahali pa Mshulami anadhihirisha upendo wake kwa Waisraeli. Katika matini yetu, Israeli wamesimamiwa na Sulemani. Kuteuliwa kwa Waisraeli na Mungu kati ya jamii zingine nyingi, kunalinganishwa na uteuzi wa Mshulami na Sulemani kati ya wasichana wengine wengi kama inavyobainika katika 8:10 kwamba - "ndipo nikawa machoni pake kama mtu aliyepata amani." Waisraeli walikuwa na amani kwa sababu walifahamu kwamba Mungu alikuwa pamoja nao hata walipokuwa katika jangwa wakielekea katika nchi waliyoahidiwa (Kanani) na Mungu.

(36): Shamba langu la mizabibu, lililo
langu mimi, li mbele yangu.
(8:12).

Binti Mshulami analilinganisha shamba lake la mizabibu na shamba alilokuwa nalo Sulemani huko Baal-hamoni. Sulemani alilikodisha shamba lake kwa walinzi/wakulima kwa vipande elfu vya fedha. Hili la Sulemani ni shamba halisi (8:11). Kinyume na hivyo, Mshulami anadai kwamba hatakodisha shamba lake ambalo liko mbele yake.

Shamba la Mshulami (mpenzi wa Sulemani) si shamba halisi bali ni jazanda iliyotumika kujirejelea yeye mwenyewe. Amejitoa kuwa mpenzi wa Sulemani. Binti huyu anakiri kwamba Sulemani amekaribishwa kusherehekea matunda ya shamba lake. Wale waliolitunza shamba hilo watapokea vipande mia mbili vya fedha - hawa ni ndugu zake Mshulami waliomwekea vikwazo tangu zamani asiolewe akiwa mdogo (1:6 na 8:8-9). Sulemani anaambiwa ahifadhi vipande vyake elfu vya fedha kumaanisha kwamba ako huru kutumia matunda ya shamba lile la Mshulami pamoja naye. Sulemani ni mshirika katika ndoa na Mshulami na kwa hivyo urembo ambao Mshulami aliuhifadhi kwa muda mrefu kwa ajili ya Sulemani, sasa Sulemani ako huru kuufurahia.

Katika jazanda hii, uhusiano kati ya Kristo na Kanisa unadhihirishwa kwani yeye (Kristo) ndiye mzabibu wa kweli kama ilivyoandikwa katika Yohana Mtakatifu 15:1. Hii ni harusi kati ya Kristo na Kanisa. Sulemani anafananishwa na Kristo ilhali Mshulami anafananishwa na Kanisa ambalo ni waumini. Kulingana na dini ya Ukristo, Yesu alijitoa bure kwa ukombozi wa ulimwengu kutoka dhambini na katika mfano huu wa (36), tunaona Mshulami akijitoa bure kwa Sulemani. Vilevile, kifungu hiki kinafasiriwa kama upendo kati ya Mungu na Sulemani au Mungu na taifa la Israeli ambapo Mshulami anachukua nafasi ya Mungu ilhali Sulemani anawakilisha taifa la Israeli

### 4.4 Hitimisho la *Wimbo Ulio Bora* kwa Mkabala wa Kidini

Kwa kuzingatia mkabala wa kidini, jazanda za *Wimbo Ulio Bora* zimetumiwa kumsifu Mungu pamoja na wema wake. Aidha, zimetumiwa kuonyesha uhusiano wa upendo kati ya Sulemani na Mungu na kati ya Mungu na Israeli. Upendo kati ya Mungu na Israeli umefananishwa na upendo kati ya Bwana arusi na Bibi arusi ambapo Sulemani ametumiwa kama Bwana arusi ilhali Mshulami ametumiwa kama Bibi arusi. Katika wimbo huu, kuna hali ya ubadilishanaji majukumu. Kuna sehemu nyingi ambazo Sulemani kama mhusika anachukua nafasi ya Mungu na kunazo chache ambazo zinamchora Mshulami kama kiashiria cha Mungu. Kwa jumla, maana ya ndani ya jazanda hizi ni kueleza uhusiano kati ya Wakristo (waokovu) na Mungu. Waokovu wanafananishwa na Mshulami ilhali Sulemani ametumiwa kuashiria Mungu. Yerusalemu mpya ni mji uliotumiwa kuashiria mahali ambapo waokovu wanatarajia kuishi pamoja na Mungu milele na milele; mbinguni.

Kulingana na mtazamo huu wa kidini, kitabu hiki ni cha kidini kabisa; kinaendeleza maudhui ya kidini na kimenuiwa kuwaleta wakristo karibu zaidi na Mungu wao.

### 4.5 Mkabala wa Kijamii wa Jazanda za *Wimbo Ulio Bora*

*Wimbo Ulio Bora* ni kitabu cha dini ya Kikristo. Kutokana na ukweli huu, tulitarajia kwamba dhana za kimsingi kabisa katika dini hii zingetajwa na kurejelewa mara kwa mara katika wimbo huu. Dhana hizo ni kama vile Mungu, Yehovah, BWANA, roho, utakatifu, malaika miongoni mwa nyingine. Hata hivyo, hatukuyafikia matarajio yetu hayo kwani tulipata kinyume cha mambo kabisa kwa sababu kitabu hiki kimezipuuza dhana hizo muhimu katika dini ya Kikristo. Katika kitabu kizima, Mungu hajatajwa hata mara moja. Sifa hii inakinyima kitabu hiki mtazamo wa moja kwa moja wa kidini. Basi, inakuwa rahisi kufafanua jazanda katika kitabu hiki kwa mkabala wa kijamii. Ufuatao ni mjadala wa mifano ya jazanda ambazo zimefasiriwa kwa kufuata mkabala wa kijamii:

(37): Ua la uwandani (2:1a).

Ua ni sehemu ya mmea. Mara nyingi ua hutumika kurejelea sehemu ya mmea ambayo huvutia macho kwa sababu ya rangi yake iliyo tofauti na sehemu zingine za mmea. Ua huvutia wadudu na hasa nyuki. Ua lililokua uwandani huonekana kwa mbali na watu au viumbe wengine. (Rejelea maelezo zaidi katika mfano wa 23). Jazanda hii inanaweza kutumiwa na msichana aliyefahamu kwamba wanaume wanamtamani na kwa hivyo akaanza kujitapia urembo wake. Pia maneno haya yatasemwa na msichana anayemhakikishia rafikiye wa kiume jinsi anavyyowavutia wanaume wengi. Aidha, yanaweza kuwa msichana huyo anajaribu kumshawishi mwanaume huyo kwa vitisho ili atilie maanani urafiki wao kwani anaweza akachukuliwa na mwanaume mwingine wakati wowote kwa vile kuna wengi wanaomtamani.

(38): Nyinyoro ya mabondeni (2:1b)

Kulingana na TUKI (1981), nyinyoro ni aina ya mmea wenye shina kama la kitunguu na unaozaa maua mekundu. Sifa muhimu katika mmea huu hasa uwapo bondeni ni kwamba haunyauki. Wakati wote maua yake huvutia kwa sababu kule bondeni, maji (unyevu) huweko kwa wingi katika misimu yote.

Maneno haya yatasemwa na msichana aliyempenda mvulana (mwanaume) kumaanisha kwamba aidha, urembo/uzuri wake haufifii au mapenzi yake kwa mwanaume huyo hayapungui katu. Maneno haya yatakuwa kama hakikisho la jinsi msichana/mwanamke huyo anavyompenda mwanaume anayeambiwa maneno hayo.

(39): Hua wangu… (2:14).

Katika kiambatisho chetu, maneno haya yalinenwa na Mshulami akimnukuu Sulemani. Tunapoiangalia jazanda hii kwa mtazamo wa kijamii, maneno haya yanaweza kusemwa na mwanaume akimsifu rafikiye wa kike akubali matakwa yake. Kwa kumrejelea kama hua, atakuwa anamaanisha kwamba msichana huyo ni mpole, mtulivu na asiyetenda madhara yoyote kama alivyo ndege aina ya hua. Aidha, maneno haya yatasemwa na mume akimchangamsha mkewe katika hali ya kumhakikishia kwamba angali anampenda.

Hii ndiyo sababu hapo chini (2:14 b-d) katika kiambatisho, anasema kwamba angependa kuona uso wake na kuisikia sauti yake kwa maana sauti yake ni tamu na uso wake ni mzuri. Wasifu huu pia wamaanisha kuwa mke huyo apendeza kwa sauti na kuvutia kwa urembo.

(40): Tukamatie mbweha,
Wale mbeha wadogo,
Waiharibuo mizabibu,
Maana mizabibu yetu
yachanua.
(2.15).

Kutokana na kiambatisho chetu, tunafahamu kwamba Mshulami (mpenzi wa Sulemani) amefungwa na shughuli za kutunza shamba la familia yao la mizabibu. Hii ndiyo sababu hapati muda wa kuonana na mpenzi wake Sulemani. Maneno haya yatasemwa na wapenzi ambao wanahitaji sana kuonana ili wafanye mipango inayoambatana na uchumba wao au ndoa yao. Hata hivyo, shughuli za kikazi au za kinyumbani au hata za kimasomo zinatinga miadi yao. Kwa hivyo, wanaomba shughuli hizo zipunguzwe na zikomeshwe na wale wanaohusika ili wawe na muda wa kuwa pamoja. Pia, maneno haya yatasemwa kama malalamishi kuhusu watu wanaopinga mapenzi yao; wanaweza kuwa wanafamilia au marafiki kwani kikulacho ki nguoni mwako. Wapenzi hawa wanawaona wale wanaojaribu kuingilia mipango yao ya kimapenzi kama maadui wakubwa wasiowatakia mema hata kidogo.

(41): Bustani iliyofungwa ni umbu
langu, bibi arusi,
(4:12a).

Maneno haya yatasemwa na bwana harusi kwa kumrejelea bibi harusi kama bustani iliyozungukwa na ua (iliyofungwa). Hili litakuwa ni onyo kwa wanaume ambao wangefikiria kumfanyia mzaha wa kimapenzi bibi harusi bila kufahamu kuwa ana mwenyewe.

(42): Kijito kilichofungwa (4:12b)

Bibi arusi anafananishwa na kijito kilichofungwa ili maji yake yasitumiwe na wapita njia. Bwana harusi anatoa onyo kwa wanaume kutomchezea bibi arusi kwani ni mkewe. Vilevile, maneno haya yatasemwa na mke akitahadharisha wanawake wengine dhidi ya kumchezea bwanake kwani yeye ni mumewe na anamheshimu.

(43): Chemchemi iliyotiwa muhuri (4:12c)

Kutia kitu muhuri ni kuonyesha kuwa kimekuwa milki ya mwenyewe au ya wenyewe na kutoka wakati huo, watu wengine hawana uhuru kukitumia bila ruhusa ya mwenyewe au wenyewe. Maneno haya yatasemwa na mume au mke kuonya wengine kuwa mkewe au mumewe ana mwenyewe. Yeye ni mke au mume wa mtu. Pengine muhuri wanaweza kuwa pete kama ishara ya uchumba, kuoa au kuolewa.

(44): Machipuko yako ni bustani ya
komamanga,
Yenye matunda mazuri..........
Na miti yote iletayo ubani ...........
(4:13-14).

Sulemani anamtwika mpenzi wake wa moyo sifa za wema (uzuri) chungu nzima. Jazanda hizi zitatumiwa na mwanaume kwa mwanamke kama njia ya kusifu wema wake ili atongozeke. Vilevile, mume anaweza kumwambia mkewe maneno haya kama njia ya kumhakikishia mapenzi yake. Matunda mazuri yanafananishwa na matendo, tabia na mienendo ya mke wa mtu kwa nia ya kumsifu ili aendelee kuwa mzuri zaidi.

(45): Wewe ndiwe kisima changu cha maji yaliyo hai. (4:15b).

Jazanda hii inanaweza kusemwa na mwanaume anayetafuta mapenzi kwa mwanamke kumwonyesha jinsi anavyompenda na kuridhika tangu akubali kuwa mpenzi wake. Mume pia atamwambia mkewe akijaribu kumwonyesha jinsi anavyopata faraja kwake na furaha wakati wowote anapomwona. Aidha, wachumba wanaweza kuhakikishiana mapenzi yao mmoja kwa mwenzake kwa kutumia maneno hayo kwa kulinganisha na kisima kisichokauka kinavyowaridhisha watumiaji wa maji yake. Yeyote atakayeitumia jazanda hii hasa katika nyanja ya mapenzi, atakuwa na nia ya kumwonyesha mwenzake vile ambavyo hawezi kuota mapenzi kwa mwanamke au mwanaume mwingine kwa sababu ameridhika na huyo mmoja.

(46): Wako malkia sitini, na masuria
themanini,
Na wanawali wasiohesabika;
Hua wangu, mkamilifu wangu, ni
mmoja tu,
Mtoto wa pekee wa mamaye.
(6:8-9).

Malkia, masuria na wanawali wasiohesabika ni mifano ya wapenzi, wanawake au marafiki wengine wanaoweza kupatikana badala ya yule mmoja. Mume anaweza kumhakikishia bibi upendo wake kwa kumwambia maneno hayo. Vilevile, iwapo kumetokea utengano kwa muda fulani kutokana na migogoro ya kinyumbani, mume anapokwenda kumshawishi mke arudi nyumbani, anaweza kutumia maneno hayo yaliyojaa ushawishi. Mvulana anaweza kutumia maneno haya kwa msichana anapomshawishi kumwonyesha jinsi alivyo tofauti na wengine wote katika kijiji, chuo au mahali pa kazi.

(47): Mwako wake ni mwako wa moto, (8:6e).

Hapa mapenzi yanasemekana kuwaka kama moto. Mchumba mwanaume anaweza kumwambia rafikiye wa kike kwamba mapenzi yake yanawaka kama moto; yanachoma. Mwanaume huyu anaweza kudai kuwa anachomwa na mapenzi ya mwanamke huyu hadi moyoni na ndio sababu hawezi kujizuia kumwambia kuwa anampenda. Maneno haya pia yanaweza kutumiwa na kila mmoja wa wachumba kuonyesha tamaa aliyonayo kwa mwenzake.

(48): Na miali yake ni miali ya
Yahu
(8:6f).

Maneno haya si tofauti sana na yale yaliyotangulia kusemwa katika mfano wa (47)). Huu ni msisitizo wa athari ya mwako wa mapenzi ya mchumba. Miali hii inalinganishwa na miali ya moto wa Yahu (Mungu) ambao unarejelewa kama ziwa la moto. Haya yametajwa katika kitabu cha Ufunuo wa Yohana 19:20, 20:10 na 21:8. Maneno haya yanaweza kusemwa na mchumba akimweleza jinsi asivyoweza kustahimili tena kuwa mbali na mwenziwe; yaani hawezi kujithibiti tena. Ni lazima wafunge ndoa. Hii ndiyo sababu Sulemani aongeza katika *Wimbo Ulio Bora* (8:7) kwamba sio moto unaoweza kuuzimisha upendo wala si mito inayoweza kuuzamisha upendo. Huu ni upendo mkuu usiodidimika.

(49): Mimi nalikuwa ukuta,
Na maziwa yangu kama minara;
Ndipo nikawa machoni pake
Kama mtu aliyeipata amani
(8:10)

Maneno haya yatasemwa na mke aliyeolewa hivi karibuni kwa maana ya kumpa pole bwanake kwa "kazi ngumu" aliyoifanya ya kumtafuta na kumfuata walipokuwa wakichumbiana. Hapa asema kuwa alikuwa ukuta; yaani haikuwa rahisi kumpata mke huyo kutokana na kazi alizopewa nyumbani pamoja na vikwazo alivyowekewa nyumbani na wazazi wake. Kwa upande mwingine, bibi huyu anawahongera kaka zake (familia yake) kwa kumwekea vikwazo na kumlea hadi utu uzima. Walimlea kwa njia nzuri hadi akawa kivutio kwa wanaume. Hii ndiyo maana anaahidi kwamba wayalindao matunda (waliomlea na kumtunza utotoni) watapata vipande mia mbili vya fedha kwa kazi nzuri waliyoifanya (8:12).

(50): Shamba langu la mizabibu, lililo
langu mimi, li mbele yangu.
(8:12)

Jazanda hii itatumiwa na mvulana kwa kumrejelea msichana aliyempenda au mvulana mchumba kwa msichana mchumba wake au mume kwa mkewe. Vilevile, yanaweza kusemwa na msichana mchumba kwa mvulana mchumbawe, au mke kwa mumewe. Kwa vyovyote vile, anayeyasema maneno haya kwa mwezake, atakuwa na nia ya kuonyesha jinsi anavyompenda na hivyo kummiliki; anamchukua kama milki yake ya kibinafsi. Ni msisitizo wa umilikaji; hili ni onyo kwa wale ambao wangedhani kuwa hana mwenyewe.

Aidha, maneno haya yatasemwa na msichana huku akijirejelea yeye mwenyewe kumaanisha kwamba amekomaa na kuwa mtu mzima. Huenda awaambie wazazi au umbu zake ambao labda wanamwona akiwa bado mtoto asiyefaa kuingilia mapenzi. Atawahakikishia kuwa anawajibika na kujitunza na kuuelewa ulimwengu kwa kuyatumia maneno hayo. Kutokana na maneno hayo, inaonyesha kuwa uamuzi atakaoufanya ni wake mwenyewe na wala hataki kuamriwa na yuko tayari kwa lolote lile litakalotokana na uamuzi alioufanya. Huyu ni kijana anayetafuta uhuru wa kiuamuzi.

### 4.6 Jazanda za *Wimbo Ulio Bora* na Miktadha ya Kijamii

Kutokana na utafiti wetu, tuligundua kwamba fasiri za jazanda za *Wimbo Ulio Bora* kwa mkabala wa kijamii (wa kawaida) kama inavyodhihirika katika sehemu ambayo tayari tumekwishaijadili ya (4.5), zinaweza kutumika katika miktadha mahsusi ya kijamii. Tumeiainisha miktadha hiyo ya kijamii katika sehemu tatu kama ifuatavyo:

(i) Utongozaji.

(ii) Uchumba.

(iii) Ndoa.

Katika sehemu hii, tuliongozwa na nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano kwa kufuata msingi uliowekwa na Hymes (1974) wa akronimu ya MWALEKIHAMKANYA. Kama tulivyokwishasema katika sehemu za 2.2.3 na 3.6, vipengele ambavyo hasa vilituongoza katika nadharia hii ni mandhari, washiriki, lengo, kitendo/vitendo, hali, msimbo na nyanja. Vipengele hivi vilituongoza katika kuchanganua miktadha ya kijamii ambayo hutokea katika hali halisi ya maisha ya kijamii.

#### 4.6.1 Utongozaji

Utongozaji ni hali ya mvulana/msichana, mume/mke kumshawishi msichana/mvulana, mke/mume ili akubali kuwa rafiki yake. Wakati wa utongozaji, maneno matamu ya kupumbaza na kusifu huweza kutumiwa. Uvumilivu pia huhitajika katika jambo hili. Jazanda zifuatazo zinapoangaliwa kwa mtazamo wa kijamii, zinaweza kutumika katika muktadha wa utongozaji.

(51): Ua la uwandani (2:la).

Maneno haya yanaweza kusemwa ana kwa ana na msichana jasiri kwa mvulana aliyemwomba urafiki. Aidha, msichana anaweza kumwandikia barua au kumtuma rafiki yake. Yanaposemwa, maneno haya yanalenga kumzindua mvulana kuhusu urembo wa msichana anayehusika na kwamba wakati wowote anaweza kuchukuliwa na mvulana mwingine iwapo mvulana anayehusika hazinduki. Hii ndiyo sababu huenda msichana aseme kuwa yeye ni ua la uwandani; yaani anaonekana na kutamaniwa na wavulana wengi kutokana na uzuri wake.

(52): Nyinyoro ya mabondeni. (2:1b).

Maneno haya yanaweza kusemwa na msichana kwa rafiki yake mvulana. Msichana anaweza kumwambia wakiwa pamoja, kupitia kwa barua au simu. Lengo la maneno haya litakuwa kumhakikishia mvulana jinsi anavyompenda. Kama nyinyoro ya mabondeni ambayo hainyauki, mapenzi ya msichana huyo kwa mvulana rafiki yake hayapungui wala hayataisha kamwe. Pia, msichana anaweza kutumia maneno haya kudhihirisha jinsi alivyoadimika; ilivyo vigumu kumpata yeye sawa na ilivyo vigumu kupata nyinyoro ya mabondeni kwani imezungukwa na mimea mingine mingi kutokana na unyevu ulioko bondeni.

(53): Machipuko yako ni bustani ya
komamanga,
Yenye matunda mazuri…
Na miti yote iletayo ubani.
(4:13-14).

Haya ni maneno yanayosifu na yenye vishawishi. Yanaweza kusemwa na mvulana anyejaribu kumshawishi msichana akubali matakwa yake ya kimapenzi. Hapa atakuwa akimtwika sifa za uzuri na wema ili ampumbaze, amleweshe kimapenzi na kumfunga macho. Maneno haya yanapotumika, yatamshawishi msichana na ajihisi kuwa anapendwa kweli kweli. Maneno haya yanaweza kusemwa faraghani, mahali wazi au yakatumwa kama ujumbe mfupi wa rununu.

(54): Kisima changu cha maji yaliyo hai...(4:15b)

Haya ni maneno ya kushawishi. Mvulana/mwanaume anaweza kumwambia msichana/mwanamke maneno haya kuonyesha jinsi kiu chake hukatika wanapoonana. Jinsi maji ya kisima yanavyokata kiu, ndivyo mwanaume huyo anaweza kukiri vile anavyomtamani na kuridhika na mapenzi ya huyo mwanamke rafiki yake. Wanaweza kuwa faraghani, aandike barua au atume ujumbe wa rununu au kwa mtandao.

(55): Wako malkia sitini, na masuria
themanini
Na wanawali wasiohesabika;
Hua wangu, mkamilifu wangu, ni
mmoja tu,
Mtoto wa pekee wa mamaye.
(6:8-9).

Malkia, masuria na wanawali ni vitengo mbalimbali vya wanawake. Jazanda hizi zinasimamia wanawake wengine wengi ambao wanaweza kuwa warembo na wazuri lakini mwanaume anakiri kwamba wema na uzuri wao haufikii ule wa mpenzi wake aliyemchagua. Anaweza kudai kwamba hakuna mwingine kama msichana huyu katika urembo na wema. Maneno haya yanapotumiwa, yanaonyesha jinsi mwanaume huyo alivyofanya uamuzi wa dhati na si rahisi kwake kutekwa na mwanamke mwingine.

(56): Mwako wake ni mwako wa moto

(57): Na Miali yake ni miali ya
Yahu,
(8:6).

Jazanda ya "mwako wa moto" na "miali ya Yahu" zimetumiwa kulinganisha ushawishi (nguvu za mapenzi) na mchomo wa mapenzi ya msichana. Haya yatatamkwa na mvulana/mwanaume kwa msichana kuthibitisha jinsi ambavyo hawezi kuishi bila mapenzi ya msichana huyo anayempenda. Kwa kawaida, wanaume huwa wana mazoea ya kuwapumbaza wasichana/wanawake kwa maneno matamumatamu huku wakiwasifu ili waweze kukubali matakwa yao ya kimapenzi. Basi, jazanda hizi za "mwako" na 'miali" kwa pamoja zinaashiria kina cha urembo na uvutiaji kwa upande wa msichana/mwanamke. Nia ya maneno haya ni kumfanya msichana/mwanamke huyo ajihisi kwamba ndiye mrembo zaidi na ndiyo maana akachaguliwa yeye kati ya wengine wengi.

(58): Shamba langu la mizabibu, lililo
langu mimi, li mbele yangu.
(8:12a).

Maneno haya yanaweza kusemwa mara mbili. Kwanza, yatasemwa na msichana kwa mvulana au mvulana kwa msichana. Mpenzi hapa analinganishwa na shamba la mizabibu na hali hii inaonyesha anavyompenda mwenziwe mpaka kiwango cha kumfanya milki yake; kwa hivyo hawezi kumwachilia. Anasisitiza kwamba shamba hilo li mbele au chini ya uangalifu wake.

### 4.6.2 Uchumba

Uchumba ni makubaliano kati ya mume na mke wanaotaka kuoana. Kwa kawida, uchumba hutanguliwa na utongozaji kisha utongozaji hufuatia uvutiaji wa macho. Fasiri za jazanda zifuatazo kwa mtazamo wa kijamii zinaweza kutumika katika muktadha wa uchumba kama inavyobainika katika mifano ifuatayo:

(59): Mimi ni nyinyoro ya mabondeni. (2:1b).

Sifa kuu ya nyinyoro ya mabondeni ni kutokauka kwani kuna unyevu misimu yote. Aidha, maumbile ya mmea huu huuwezesha kuhifadhi maji kwa muda mrefu. Kwa msingi huo, msichana aliyeingia uchumbani na mvulana atamhakikishia mapenzi yake kwa maneno hayo. Anaweza kumwambia mvulana maneno haya wakiwa katika mandhari ya miti (msitu) na mabonde. Basi, msichana atakuwa amejilinganisha na ua la nyinyoro lililokulia bondeni ambako haliwezi kukauka.

(60): Hua wangu (2:14).

Hua ni ndege mpole na asiye madhara. Katika Biblia, hua hunasibishwa na amani na utulivu. Mvulana anaweza kumwambia msichana maneno haya kwa kumlinganisha na hua katika upole na kutokuwa na madhara yoyote. Hizi ni sifa nzuri zilizolenga kuimarisha uchumba kati ya wachumba hao wawili.

(61): Tukamatie mbweha.
Wale mbweha wadogo,
Waiharibuo mizabibu,
Maana mizabibu yetu
yachanua.
(2:15).

Maneno haya yanaweza kusemwa na wachumba wote wawili katika hali ya maombi kwa Mungu wakimsihi awajalie na awaepushie maadui wa uchumba wao.

Maadui hawa ndio wanaorejelewa kama mbweha wanaoharibu mizabibu. Maadui wa uchumba wanaweza kuwa watu wa familia zao, marafiki au tofauti za mila, desturi, rangi na hadhi za kijamii. Mizabibu ni kiashiria cha uchumba wao. Tamaa yao ni kuona uchumba wao ukinawiri na kukua siku baada ya nyingine kuelekea katika ndoa ambayo ndiyo kilele cha mapenzi.

(62): Bustani iliyofungwa ni umbu
langu, bibi arusi,
(4:12a).

Baada ya kukubali urafiki, uchumba huanza. Huenda ishara ya uchumba iwe ni pete ivaliwayo kwenye kidole. Maneno haya yanaweza kusemwa na mvulana/mwanaume aliyemchumbia msichana kama tahadhari kwa walimwengu kuwa 'wasimchezee' msichana huyo kwani tayari ameshachumbiwa.

(63): Kijito kilichofungwa (4:12b).

(64): Chemchemi iliyotiwa muhuri (4:12c).

Jazanda hizi mbili zitatumiwa katika muktadha wa uchumba sawa na vile ambavyo jazanda iliyotangulia (mfano wa 62) inavyoweza kutumika.

(65): Machipuko yako ni bustani ya
komamanga,
Yenye matunda mazuri...
(4:13).

Kwa kusifu matendo, maneno, urembo na tabia za mpenzi wake, mvulana mchumba anaweza kutumia maneno haya. Haya ni maneno yenye nguvu za ushawishi wa kumfanya msichana asimtamani mwingine. Mandhari ya maneno haya yanaweza kuwa msitu au kwenye mbuga au katika bustani yenye kila aina ya maua.

(66): Wewe ni kisima cha maji yaliyo hai...(4:15b).

Mtu akiyanywa maji yaliyo hai, yasemekana haoni kiu tena; (Yohana 4:10-14). Maneno haya yanaweza kusemwa na wachumba wakidhihirishiana jinsi wanavyopata furaha na faraja punde tu wanapoonana au kuwazana.

Mvulana anaweza kumwambia msichana maneno haya kumwonyesha jinsi anavyopata amani kwa sababu ya urafiki wao na msichana anaweza akayatumia maneno haya kwa nia iyo hiyo. Bila shaka, haya ni maneno ya kupumbazana.

(67): Wako malkia sitini, na masuria
themanini,
Na wanawali wasiohesabika;
Hua wangu, mkamilifu wangu, ni
mmoja tu,
Mtoto wa pekee wa mamaye.
(6:9).

Malkia sitini, masuria themanini na wanawali wasiohesabika ni jazanda ambazo zitatumiwa na mvulana/mwanamume kwa mchumba wake kumwonyesha kwamba hawezi kumlinganisha na msichana au mwanamke mwingine kamwe. Maneno haya yatalenga kumkumbusha msichana kwamba alichaguliwa kati ya wasichana/wanawake wengi; kwa hiyo anapendwa na kuthaminiwa sana.

(68): Mwako wake ni mwako wa moto (8:6c).

Hatima ya uchumba ni ndoa. Wakati mwingine huenda ndoa ifikiwe haraka kwa sababu ya wachumba kukosa kuthibiti hisia zao za kimapenzi. Hali hii inathibitishwa na jazanda hii ya mwako wa moto. Mvulana anaweza kumwambia mvulana mwenzake huku akimrejelea msichana mchumba wake kumaanisha kwamba mapenzi yake yanamchoma kama moto uchomavyo na kwa hivyo hawezi kujithibiti tena au kustahimili kukaa mbali naye. Maneno haya yatasemwa katika kilele cha uchumba wao. Jazanda inayofuata ya miali yake ni miali ya Yahu (8:6f) katika kiambatisho, itatumiwa kwa lengo hilo pia.

(69): Shamba langu la mizabibu, lililo
langu mimi, li mbele yangu.
(8:12).

Shamba la mizabibu ni jazanda ambayo inanaweza kutumiwa na mvulana kumrejelea mpenzi wake. Zabibu ni matunda matamu ambayo hapa yanafananishwa na utamu wa mapenzi ya msichana anayehusika katika *Wimbo Ulio Bora*. Msichana mwenyewe pia ataitumia jazanda hii kuurejelea mwili wake, urembo wake na jinsi anavyoutunza ili uweze kumvutia kabisa mchumba wake.

### 4.6.3 Ndoa

Ndoa ni maafikiano kati ya mwanaume na mwanamke waliokubaliana kuishi pamoja kama mume na mke ili waunde familia yao. Kwa bahati baya, asasi hii hukabiliwa na matatizo mengi kama vile kutoaminiana, utengano na kutalakiana. Maneno matamu na tabia jema ni ala ambazo zinafaa kutumiwa mara kwa mara ili kuujenga uaminifu kati ya wanandoa. Jazanda zifuatazo zinaweza kutumiwa katika muktadha wa ndoa:

(70): Mimi ni nyinyoro ya mabondeni. (2:1b).

Katika harakati za kumhakikishia bwana imani kwake, bibi anaweza kutumia maneno haya. Kwa kujifananisha na nyinyoro ya bondeni, atakuwa akimaanisha kwamba upendo wake kwa mumewe haudidimii wala hauwezi kwisha kama ambavyo nyinyoro ya bondeni isivyonyauka. Huenda iwe mumewe alimshuku mkewe kuwa na jicho la nje, lakini bibi akamjibu kwa maneno hayo.

(71): Hua wangu (2:14).

Kama tulivyotangulia kusema, ndoa ni asasi ya kijamii ambayo hukubwa na matatizo mengi. Hali hii huashiria haja ya kutunza uhusiano kati ya mke na mume. Itabidi maneno mazuri yatumiwe mara kwa mara ili kujenga uhusiano mwema. Jazanda hii inaweza kutumiwa na mume akimwambia mkewe. Lengo hapa linaweza kuwa kumsifu bibi ili awe na furaha kwa kumfananisha na hua aliye mpole, mtulivu, mwenye amani na asiye madhara. Hata hivyo, maneno kama haya hayawezi kusemwa wakati ambapo kuna migogoro kati yao bali ni wakati wa furaha na uchangamfu.

(72): Tukamatie mbweha
Wale mbweha wadogo,
Waiharibuo mizabibu,
Maana mizabibu yetu
yachanua
(2:15).

Ndoa ina maadui wengi. Hawa maadui ndio wanaotajwa kama mbweha. Katika sherehe ya harusi, maharusi wanaweza kufanya ombi hili kwa Mungu awajalie heri katika ndoa yao. Maadui wanaweza kuwa marafiki, wazazi na familia zao kwa jumla. Vilevile, iwapo tayari kumetokea mafarakano katika ndoa na wakatengana, wanaporudiana, maneno haya yanaweza kutumiwa yawe kama mwanzo wa ufufuo wa ndoa hiyo iliyofifia baada ya misukosuko.

(73): Bustani iliyofungwa ni umbu
langu, bibi arusi,
(4:12a).

(74): Kijito kilichofungwa. (4:12b).

(75): Chemchemi iliyotiwa muhuri. (4:12c).

Jazanda hizi tatu yaani bustani iliyofungwa, kijito kilichofungwa na chemchemi iliyotiwa muhuri, zinaweza kutumika kwa pamoja au kwa lengo moja. Kwa mfano: Maneno bustani iliyofungwa huenda yakatamkwa mbele ya watu/waumini na mume wakati wa kufunga ndoa. Vilevile, mume anaweza akamtaja bibi yake kama kijito kilichofungwa hivi kwamba wapitanjia hawana ruhusa kutumia maji yake na vivyo hivyo kwa chemchemi iliyotiwa muhuri. Sifa hizi zinazoambatanishwa na bustani, kijito na chemchemi zinaashiria umilikaji hasa hadharani kama vile kanisani. Maneno haya yakisemwa na mume, atakuwa na lengo la kuwatahadharisha wanaume dhidi ya 'kumtania' bibi yake. Aidha, lengo litakuwa lilo hilo iwapo maneno hayo yatasemwa na mke akimrejelea mumewe.

(76): Machipuko yako ni bustani ya
komamanga,
Yenye matunda mazuri...
(4:13).

Maneno, tabia na mienendo ni mambo yanayomvutia sana mume kwa mke wake. Basi mume anaweza kutumia maneno haya kumsifu mkewe kwa tabia yake nzuri ili kumtia moyo aendelee kuchipuka yaliyo mema tu. Hata hivyo, tunachukulia kwamba maneno haya yatasemwa tu na mume anayejivunia mkewe. Vilevile, mke anayejivunia mumewe anaweza kuyatumia maneno haya kuonyesha jinsi anavyoyafurahia matendo, tabia na mienendo yake.

(77): Wako malkia sitini, na masuria
themanini,
Na wanawali wasiohesabika;
Hua wangu, mkamilifu wangu, ni
mmoja tu,
Mtoto wa pekee wa mamaye
(6:8-9).

Mume atamwambia mke maneno haya hasa baada ya mgogoro wa kinyumbani kutokana na kutoaminika kwa mume. Inawezekana mume anashukiwa kuwa na vimanda hapa na pale. Katika kujitetea, mke anaweza kwambiwa maneno hayo ili ashushe hasira. Haya ni maneno ya kumhakikishia kwamba bado yuapendwa na asitie shaka kwani wananwake wengi hawawezi kumfikia katika wema na urembo.

(78): Mimi nalikuwa ukuta.
Na maziwa yangu kama minara;
Ndipo nikawa machoni pake
Kama mtu aliyeipata amani.
(8:10)

Katika ndoa, kuna kumbukumbu nyingi za mambo yalivyokuwa tangu nyakati za utongozaji, urafiki, uchumba na ndoa. Mke anaweza kumkumbusha mumewe jinsi yeye (bibi) alivyokuwa mgumu kwa kuwakatalia mbali wanaume wengine. Pia, alikuwa mgumu hivi kwamba hata mumewe katika ujana wao hakuwa akimpata kwa urahisi. Hata hivyo, katika kuadimika huko, aliweza kudumisha hadhi yake kama msichana mwenye tabia nzuri, hàli ambayo ilimvutia zaidi kwa mume huyo. Maneno haya yanaweza kusemwa nyumbani katika hali ya uchangamfu wakati wa mapumziko ambapo wanandoa hawa wanaweza kukumbuka matukio ya kale.

(79): Shamba langu la mizabibu, lililo
langu mimi, li mbele yangu.
(8:12a).

Maneno haya huenda yatamkwe na mume au mke kila mmoja akielezea hisia zake kwa mwenzake. Mume anakiri kwamba shamba lake la mizabibu (mkewe) ni lake na liko mikononi mwake, yaani analitunza. Kwa njia hiyo, mke naye anaweza kuonyesha mapenzi yake kwa mumewe kwa kumrejelea kama shamba lake. Lengo la kutumia jazanda hii ni kounyesha kwamba kila mmoja wa wanandoa hao anamhitaji mwenzake kama msaidizi wake. Ni jukumu la mume kuona kwamba mkewe amepata mahitaji anayostahili na kwa upande mwingine, ni jukumu la mke kuhakikisha kuwa mumewe ametunzwa vizuri kwa huduma kama vile kuandaliwa chakula na kufuliwa nguo. Kila mmoja ana wajibu wake muhimu katika ndoa. Ni lazima kila mmoja ayatambue majukumu yake na kuyatimiza kwa uwajibikaji ili kufikia ukamilifu wa ndoa.

## 4.7 Hitimisho la jazanda za *Wimbo Ulio Bora* na Miktadha ya Kijamii

Japokuwa *Wimbo Ulio Bora* ni kitabu cha kidini, jazanda zilizomo zimeweza kufafanuliwa kwa kujikita katika miktadha ya kijamii. Tumehusisha jazanda hizo katika miktadha mitatu ambayo ni utongozaji, uchumba na ndoa huku tukiongozwa na nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano ya Hymes (1974). Imebainika kwamba, tajriba na haja za washiriki ndizo zinazoongoza kuamua maana itakayopewa jazanda husika ili kuwawezesha washiriki kukidhi mahitaji yao mahsusi.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Tumeigawa sura hii katika sehemu nne. Katika sehemu ya kwanza, tunaeleza muhtasari wa matokeo makuu ya utafiti. Sehemu ya pili inatoa kwa kifupi hitimisho la muradi huu. Katika sehemu ya tatu, mapendekezo yanayoambatana na matokeo ya utafiti huu yanaelezwa huku sehemu ya mwisho ikitoa mapendekezo ya utafiti zaidi kwa wasomi wa halafu.

### 5.2 Muhtasari wa Matokeo Makuu

Kutokana na utafiti tulioufanya, tuliweza kubaini mambo makuu yafuatayo:

1. Japokuwa *Wimbo Ulio Bora* ni kitabu cha kidini kwa ambavyo kimo katika Biblia takatifu, jazanda zilizomo zimetumika katika maswala yaliyo nje ya dini ya kikrsto.

2. Jazanda zilionekana kuasi Kaida ya Ushirikiano kwa kuvunja au kukiuka kanuni ya "kiasi" na ya "namna". Hali hii inazua utata wa kimaana badala ya kuupunguza kama inavyoshauriwa na Pragmatiki ya Grice (1967).

3. Jazanda kama zao la jamii, huchotwa kutoka kwa mazingira ya kijamii. Katika *Wimbo Ulio Bora*, majina mbalimbali ya miti, matunda, maua, wanyama na maumbile ya ardhi yanatajwa kurejelea hali tofauti tofauti za kijamii.

4. Ufasiri wa jazanda hutegemea tajriba, mahitaji na miktadha wanamojikuta washiriki wa matukio ya kijamii. Jazanda za Wimbo Ulio Bora zinakidhi haja tofauti tofauti (za kidini na kijamii) kwa washiriki tofauti tofauti.

5. Katika kufasiri jazanda, dhana za kizingumzwa, kifananishi na kiungo ni muhimu kufahamika

6. Ili kufanya fasiri bora ya jazanda, sharti nafasi ya ufananishaji wa sifa izingatiwe.

7. Ni rahisi wimbo huu kueleweka kwa mtazamo wa kijamii kutokana na ukweli kwamba umenyimwa viashiria vya kidini.

8. Katika wimbo huu, kuna hali ya ubadilishanaji wa majukumu. Katika sehemu nyingi, nafasi ya Mungu inachukuliwa na Sulemani ilhali katika sehemu chache, Mshulami (msichana) anaashiria Mungu.

### 5.3 Hitimisho

Kwa jumla, tuliweza kufafanua jazanda ishirini na tano. Japokuwa *Wimbo Ulio Bora* ni kitabu cha kidini, tuligundua kwamba jazanda zilizomo zinaweza kufasiriwa hata kwa mkabala wa kijamii.

Kufuatia matokeo ya utafiti huu, ilifahamika kuwa kwa kuzipa jazanda hizo mtazamo wa kijamii, fasiri zao zinaweza kutumika katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Hili liliwezekana pale tulipohusisha fasiri za jazanda hizo katika miktadha ya kijamii hususan ile ya kimapenzi. Tulijikita katika miktadha ya utongozaji, uchumba na ndoa. Aidha, ilibainika kuwa viashiria vya kidini havijapewa nafasi katika wimbo huu. Viashiria hivi ni kama vile dhana ya Mungu, roho, malaika, mtume, mtumishi wa Mungu na kadhalika. Sifa hii bainifu ilituidhinisha kuuchukua mkabala wa kijamii katika kuzifafanua jazanda zilizomo. La mno ni kwamba, jina la Mwenyezi Mungu halitajwi ko- kote katika wimbo huu wa kidini.

Matokeo yamezithibitisha nadharia tete kama tulivyokisia katika pendekezo la utafiti. (Rejelea sehemu ya 1.5). Kuhusu nadharia tete ya kwanza, tumegundua kuwa jazanda za *Wimbo Ulio Bora* zinaweza kufasiriwa kwa mikabala ya kidini na kijamii. Kuhusu nadharia tete ya pili, tulifahamu kuwa inawezekana kudhihirisha jinsi jazanda za *Wimbo Ulio Bora* zinavyoweza kutumika katika miktadha ya kijamii. Tulitumia miktadha ya utongozaji, uchumba na ndoa kudhihirisha kisio hili.

## 5.4 Mapendekezo

Aghalabu maswala ya kidini, sifa za lugha zikiwemo, hayapigiwi maswali. Hata hivyo, tulipochanganua *Wimbo Ulio Bora* kihakiki, mambo yanayohitaji kumulikwa na wanaohusika yalizuka. Hii ni kwa sababu jazanda zote tulizoweza kuzitambulisha zilikubali kuhusishwa kwenye miktadha ya kijamii hususa ile ya kimapenzi. Kwa hivyo, kutokana na matokeo ya utafiti wetu, tunatoa mapendekezo yafuatayo:

1. Wahakiki na wataalamu wa Biblia wanafaa kukitalii upya kitabu hiki cha *Wimbo Ulio Bora* ili kupima ufaafu wake kama kitabu cha kidini. Yaonekana kama kitabu hiki kiliwekwa katika Biblia (kitabu kitakatifu) kimakosa.

2. Ugumu (utata) mkubwa ulidhihirika katika kufasiri jazanda za *Wimbo Ulio Bora*. Utata huu unaweza kupunguzwa na wafasiri wa Biblia kwa kutoa miongozo mingi na ya bei nafuu (sawa na ilivyo rahisi kupata nakala za Biblia) ili iwe rahisi kwa kila msomi wa Biblia kuelewa maana ya vifungu tofauti tofauti.

3. Anwani ya kitabu hiki (*Wimbo Ulio Bora*) yafaa kuangaliwa upya na pengine iwe *Wimbo wa Sulemani au Sulemani na Mpenzi Wake* au *Ushairi wa Mapenzi*. Kwa sasa, waandishi na wahakiki wa Biblia hawajaafikiana kuhusu anwani ya wimbo huu. Kuna wale wanaouita "*Wimbo wa Sulemani*" ilhali wengine wanauita "*Wimbo Ulio Bora*". Pana haja ya kutafuta maridhiano kwa kukubaliana kuhusu anwani moja.

4. Marejeleo kuhusu ufasiri wa jazanda za kidini yalidhihirisha uhaba mkuu. Hii ni kutokana na sababu kwamba labda eneo hili la kidini limepuuzwa na wasomi. Hii ni changamoto kwa wanaisimu na wanafasihi kwa kupuuza eneo hili lenye rutuba nyingi.

5. Tunapendekeza wimbo huu utumiwe kufunzia mashairi katika shule za Sekondari na Vyuo Vikuu.

### 5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Kutokana na utafiti wetu, kuna mambo muhimu yaliyoibuka ambayo hatungeweza kuyashughulikia kwa tafsili kutokana na sababu za upeo wa utafiti wetu. Kwa hiyo, katika sehemu hii, tunapendekeza mambo yafuatayo kwa utafiti zaidi:

1. Utafiti wetu ulijikita tu katika *Wimbo Ulio Bora* tu. Tafiti zingine zinafaa kufanyiwa vitabu vingine vya Biblia hususan vile vya kishairi ili kuwe na upana wa kiuamuzi kuhusu ufaafu wa matokeo yetu.

2. Utafiti wetu umejihusisha na jazanda peke yake. Utafiti kama huu wafaa kufanywa kwa mbinu ya tashbihi ambayo imetumika kwa wingi katika *Wimbo Ulio Bora*.

3. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kwamba ufasiri wa jazanda za *Wimbo Ulio Bora* unaegemea pakubwa kwa upande wa kijamii kuliko kidini. Hivyo, pana haja ya kuchunguza maudhui ya mapenzi katika wimbo huu.

4. Katika ukusanyaji wa Data, hatukuhusisha wasomi wa Biblia. Utafiti mwingine unafaa kufanywa kwa kuwahusisha ana kwa ana wasomi na wahakiki wa Biblia ili kuwe na msingi bora wa ulinganishaji.

## MAREJELEO


Barker, K. (1995) *The NIV Study Bible*. U.S.A: Zondervan Publishing House.

Baxter, J. (1973) *Explore the Book; Volume One*.Michigan: Zondervan Publishing House.

Borton. J. (1998) *The Cambridge Companion to Biblical Interpretation*. Cambridge: Cambridge University Press.

Brown, G. (1995). *Speakers. Listeners and Communication: Explorations in Discourse Analysis*. Cambridge: Cambridge University Press.

Cross, F. na Livingstone, E. (1990) *The Oxford Dictionary of The Christian Church*. New York: Oxford University Press.

Davidson, D. (1984) *Inquiries into Truth and Interpretation*. New York: Oxford University Press.

Davis, S. (1991) *Pragmatics; A Reader*. New York: Oxford University Press.

Ebest, S. na wengine (2003) *Writing from A to Z*. Boston: Mc Graw Hill.

Fuller, R. (1981) *A New Catholic Commentary on Holy Scripture*. Nairobi: Nelson.

Goldingay, J. (1995) *Models for Interpretation of Scripture*. Michgan: William B. Eerdmans Publishing Company.

Grudy, P. (2000) *Doing Pragmatics; Second Edition*. London: Arnold.

Harmon, N. na wengine (1987) *The Interpreter's Bible; Volume 5*. Nashville: Abingdom Press.

Imbosa, R. (1990) *Jazanda Katika Ushairi Wa Muyaka*. Tasnifu ya M.A. , Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Irwin. C. (1986) *Irwin's Bible Commentary*. Philadelphia: Universal Book and Bible House.

King James Bible (1980) *Word of God*. Florida: Oxford University Press.

Lakoff, G. na Johnson, M. (1980) *Metaphors We Live By*. Chicago: The University of Chicago press.

Leech, N. na Short, M. (1981) *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*. London: Longman.

Levinson, S. (1992) *Pragmatics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Martinich, A. (1990) *The Philosophy of Language; Second Edition*. Oxford: Oxford University Press.

Mesthrie. R. (2001) *Concise Encyclopaedia of Sociolinguistics*. Oxford: Elsevier Science Limited.

Mulokozi, M. na Kahigi, K. (1979) *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Murphey, C. (1989) *The Dictionary of Biblical Literacy*. Nashville: Oliver – Nelson Books.

Nasiri, S. (1980) *Inkishafi*. Nairobi: Longman.

Roberts, C. (1992) *Language and Discrimination*. New York: Longman Publishing.

Scofield C. (1979) *The Holy Bible Concordance; New Scofield Reference*. New York: Oxford University Press.

Syambo, B. na Mazrui, A. (1992) *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Taylor, K. (1972) *The Living Bible; The Bible in Everyday Language for Everyone*. Great Britain: Tyndale House Publishers.

The Bible Societies of Kenya & Tanzania, (1977) *Biblia.*. Nairobi.

New International Version (1973) *The Holy Bible*. New York: New York International Bible Society.

Thomas, J. (1995) *Meaning in Interaction; An Introduction to Pragmatics*. New York: Longman.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es salaam: Oxford University Press.

Walibora, K. (1996) *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wallah, W. (2000) *Malenga wa Ziwa Kuu: Maswali na Istilahi za Kifasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers

Wamitila, K. (2003) *Kichocheo cha Fasihi; Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books

Wansbrough, H. (1985) *The New Jerusalem Bible*. London: Darton na Todd.

**KIAMBATISHO**

# WIMBO ULIO BORA

1 1 Wimbo ulio bora, wa Sulemani.!
2 Kubusu na anibusu kwa kinywa
chake.
Maana pambaja zako zapita divai;
3 Manukato yako yanukia vizuri;
Jina lako ni kama marhamu
iliyomiminwa;
Kwa hiyo wanawali
hukupenda.!
4 Nivute nyuma yako, na tukimbie;
Mfalme ameniingiza vyumbani
mwake.
Tutafurahi na kukushangilia;
Tutazinena pambaja zako kuliko
divai;
Ndiyo, ina haki wakupende.!

5 Mimi ni mweusi-mweusi, lakini
ninao uzuri,
Enyi binti za Yerusalemu,
Mfano wa hema za Kedari,
Kama mapazia yake Sulemani.
6 Msinichunguze kwa kuwa ni
mweusi-mweusi,
Kwa sababu jua limeniunguza.
Wana wa mamangu
walinikasirikia,
Waliniweka niwe mlinzi wa
mashamba ya mizabibu;
Bali shamba langu mwenyewe
sikulilinda.

7 Nijulishe, ee mpendwa wa nafsi
yangu,
Ni wapi utakapolisha kundi
lako,
Ni wapi utakapolilaza adhuhuri.
Kwa nini niwe kama
aliyefungiwa kidoto,
Karibu na makundi ya
wenzako?!
8 Usipojua, wewe uliye mzuri
katika wanawake,
Shika njia uzifuate nyayo za
kondoo,
Na kuwalisha wana-mbuzi wako
Karibu na hema za wachungaji.

Wenendo

Hulisha kundi lake penye
nyinyoro.†
17 Hata jua lipunge, na vivuli
vikimbie,
Unigeukie, mpendwa wangu,
Nawe uwe kama paa, au ayala,
Juu ya milima ya Betheri.†

3 1 Usiku kitandani nalimtafuta
mpendwa wa nafsi yangu,
Nalimtafuta, nisimpate.†
2 Nikasema, Haya, niondoke
nizunguke mjini,
Katika njia zake na viwanjani,
Nimtafute mpendwa wa nafsi
yangu.
Nikamtafuta, nisimpate.
3 Walinzi wazungukao mjini
waliniona;
Je! Mmemwona mpendwa wa
nafsi yangu?†
4 Kitambo kidogo tu nikiisha
kuwaondokea,
Nikamwona mpendwa wa nafsi
yangu;
Nikamshika, nisimwache tena,
Hata nilipomleta nyumbani mwa
mamangu,
Chumbani mwake aliyenizaa.†
5 Nawasihi, enyi binti za
Yerusalemu,
Kwa paa na kwa ayala wa
porini,
Msiyachochee mapenzi, wala
kuyaamsha,
Hata yatakapoona vema
yenyewe.†
6 Ni nani huyu apandaye kutoka
nyikani,
Mfano wake ni nguzo za moshi;
Afukizwa manemane na ubani,
Na mavumbi ya manukato yote
ya mchuuzi?†
7 Tazama, ni machela yake
Sulemani;
Mashujaa sitini waizunguka,
Wa mashujaa wa Israeli.
8 Wote wameshika upanga,
Wamehitimu kupigana;
Kila mtu anao upanga wake
pajani
Kwa hofu ya kamsa za usiku.
9 Mfalme Sulemani alijifanyizia
machela
Ya miti ya Lebanoni;
10 Nguzo zake alizifanyiza za fedha,
Na mgongo wake wa dhahabu,
Kiti chake kimepambwa urujuani,
Gari lake limenakishiwa njumu,
Hiba ya binti za Yerusalemu.†
11 Tokeni, enyi binti za Sayuni,
Mtazameni Mfalme Sulemani,
Amevaa taji alivyovikwa na
mamaye,
Siku ya maposo yake,
Siku ya furaha ya moyo wake.†

4 1 Tazama, u mzuri, mpenzi
wangu,
U mzuri, macho yako ni kama
ya hua,
Nyuma ya barakoa yako.
Nywele zako ni kama kundi la
mbuzi,
Wakijilaza mbavuni pa mlima
Gileadi.†
2 Meno yako ni kama kundi
waliokatwa manyoya,
Wakipanda kutoka kuoshwa,
Ambao kila mmoja amezaa
mapacha,
Wala hakuna aliyefiwa kati
yao.†
3 Midomo yako ni kama uzi
mwekundu,
Na kinywa chako ni kizuri;
Mashavu yako ni kama kipande
cha komamanga,
Nyuma ya barakoa yako.
4 Shingo yako ni kama mnara wa
Daudi,
Uliojengwa pa kuwekea silaha;
Ngao elfu zimetungikwa juu yake,
Zote ni ngao za mashujaa.†
5 Maziwa yako mawili ni kama
wana-paa wawili,
Nyuma ya barakoa yako.
Ambao ni mapacha ya paa;
Wakilisha penye nyinyoro.†

6 Hata jua lipunge, na vivuli
vikimbie,

Nitakwenda kwenye mlima wa
manemane,
Na kwenye kilima cha ubani.

7 Mpenzi wangu, u mzuri pia pia,
Wala ndani yako hamna ila.†
8 Bibi arusi, njoo pamoja nami
toka Lebanoni,
Pamoja nami toka Lebanoni.
Shuka kutoka kilele cha Amana,
Kutoka vilele vya Seniri na
Hermoni;
Kutoka mapangoni mwa simba,
Kutoka milimani mwa chui.†
9 Umenishangaza moyo, umbu
langu,
Bibi arusi, umenishangaza
moyo,
Kwa mtupo mmoja wa macho
yako,
Kwa mkufu mmoja wa shingo
yako.†
10 Jinsi zilivyo nzuri pambaja zako,
umbu langu,
Bibi arusi, ni nzuri kupita divai,
Na harufu ya marhamu yako
Yapita manukato ya kila
namna.
11 Bibi arusi, midomo yako
yadondoza asali,
Asali na maziwa vi chini ya
ulimi wako;
Na harufu ya mavazi yako
Ni kama harufu ya Lebanoni.†
12 Bustani iliyofungwa ni umbu
langu, bibi arusi,
Kijito kilichofungwa,
chemchemi iliyotiwa muhuri.†
13 Machipuko yako ni bustani ya
komamanga,
Yenye matunda mazuri, hina
na nardo,
14 Nardo na zafarani, mchai na
mdalasini,
Na miti yote iletayo ubani,
Manemane na udi, na kolezi
kuu zote.
15 Wewe ndiwe chemchemi ya
bustani yangu,
Kisima cha maji yaliyo hai,
Vijito vya Lebanoni viendavyo
kasi.†
16 Amka, kaskazi; nawe uje, kusi;
Vumeni juu ya bustani yangu,
Manukato ya bustani yatokee.
Mpendwa wangu na aingie
bustanini mwake,
Akayale matunda yake mazuri.†

5 1 Naingia bustanini mwangu,
umbu langu, bibi arusi,
Nachuma manemane yangu na
rihani,
Nala sega la asali na asali yangu,
Nanywa divai yangu na
maziwa.
Kaleni, rafiki zangu, kanyweni,
Naam, nyweni sana, wapendwa
wangu.†

2 Nalikuwa nimelala, lakini moyo
wangu u macho,
Sikiliza! Mpendwa wangu
anabisha!
Nifungulie, umbu langu, mpenzi
wangu,
Hua wangu, mkamilifu wangu,
Kwa maana kichwa changu
kimelowa umande,
Nywele zangu zina manyunyu
ya usiku.†
3 Nimeivua kanzu yangu; niivaeje?
Nimeitawadha miguu;
niichafueje?
4 Mpendwa wangu aliutia mkono
wake tunduni,
Na moyo wangu ukachomeka
kwa ajili yake.
5 Nikaondoka nimfungulie
mpendwa wangu;
Mikono yangu ilidondoza
manemane,
Na vidole vyangu matone ya
manemane,
Penye vipini vya komeo.
6 Nalimfungulia mpendwa wangu,
Lakini mpendwa wangu
amegeuka amepita;
(Nimezimia nafsi yangu
aliponena),
Nikamtafuta, nisimpate,
Nikamwita, asiniitikie.†
7 Walinzi wazungukao mjini
waliniona,

Wakanipiga na kunitia jeraha,
Walinzi walindao kuta zake
Wakaninyang'anya shela
yangu.†
8 Nawasihi, enyi binti za
Yerusalemu,
Ninyi mkimwona mpendwa
wangu,
Ni nini mtakayomwambia?
Ya kwamba nazimia kwa
mapenzi.

9 Mpendwa wa namna gani ni
mpendwa wako,
Wewe uliye mzuri katika
wanawake,
Mpendwa wa namna gani ni
mpendwa wako,
Hata wewe utusihi hivyo?

10 Mpendwa wangu ni mweupe,
tena mwekundu,
Mashuhuri miongoni mwa elfu
kumi;
11 Kichwa chake ni kama dhahabu
safi sana,
Nywele zake ni za ukoka,
nyeusi kama kunguru;
12 Macho yake ni kama hua penye
vijito,
Wakioga kwa maziwa,
wakiikalia mito iliyojaa;†
13 Mashavu yake ni kama matuta
ya rihani,
Ambayo hufanyizwa manukato;
Midomo yake ni kama nyinyoro,
Inadondoza matone ya
manemane;
14 Mikono yake ni kama mianzi ya
dhahabu,
Iliyopambwa kwa zabarajadi;
Kiwiliwili chake kama kazi ya
pembe,
Iliyonakishiwa kwa yakuti
samawi;
15 Miguu yake ni kama nguzo za
marimari,
Zilizowekwa juu ya misingi ya
dhahabu;
Sura yake ni kama Lebanoni,
Ni bora mfano wa mierezi;
16 Kinywa chake kimejaa maneno
matamu,
Ndiye mzuri sana pia pia.
Ni huyu mpendwa wangu, ni
huyu rafiki yangu,
Enyi binti za Yerusalemu.†

# 6

1 Mpendwa wako amekwenda
wapi,
Wewe uliye mzuri katika
wanawake?
Mpendwa wako amegeukia
upande upi,
Ili tumtafute pamoja nawe?†

2 Mpendwa wangu ameshukia
bustani yake,
Kwenye matuta ya rihani;
Ili kulisha penye bustani,
Ili kuchuma nyinyoro.†

3 Mimi ni wake mpendwa wangu,
naye ni wangu,
Hulisha kundi lake penye
nyinyoro.†

4 Mpenzi wangu, u mzuri kama
Tirza,
Mwenye kupendeza kama
Yerusalemu,
Wa kutisha kama wenye
bendera.†
5 Uyageuzie macho yako mbali
nami,
Kwa maana yamenitisha sana.
Nywele zako ni kama kundi la
mbuzi,
Wakijilaza mbavuni pa
Gileadi.†
6 Meno yako kama kundi la
kondoo,
Wakipanda kutoka kuoshwa;
Ambao kila mmoja amezaa
mapacha,
Wala hakuna aliyefiwa kati yao.
7 Mashavu yako ni kama kipande
cha komamanga,
Nyuma ya barakoa yako.

8 Wako malkia sitini, na masuria
themanini,
Na wanawali wasiohesabika;
9 Hua wangu, mkamilifu wangu, ni
mmoja tu,
Mtoto wa pekee wa mamaye.

Ndiye kipenzi chake aliyemzaa,
Binti wakamwona wakamwita heri;
Malkia na masuria nao wakamwona,
Wakamsifu, wakisema,

10 Ni nani huyu atazamaye kama alfajiri,
Mzuri kama mwezi, safi kama jua,
Wa kutisha kama wenye bendera?

11 Nalishukia bustani ya milozi,
Ili kuyatazama machipuko ya bondeni;
Nione kama mzabibu umechanua,
Kama mikomamanga imetoa maua.†
12 Kabla sijajua, roho yangu ilinileta
Katikati ya magari ya wakuu wangu.

13 Rudi, rudi, Mshulami,
Rudi, rudi, ili sisi tukutazame.

Kwani mnataka kumtazama Mshulami,
Kama kutazama ngoma ya Mahanaimu?

7 1 Siti msharifu, jinsi zilivyo nzuri
Hatua zako katika mitalawanda.
Mapaja yako ya mviringo ni kama johari,
Kazi ya mikono ya fundi mstadi;†
2 Kitovu chako ni kama bilauri iliyoviringana,
Na isikose divai iliyochanganyika;
Tumbo lako ni mfano wa chungu ya ngano,
Iliyozungukwa na ugo wa nyinyoro;
3 Maziwa yako mawili ni kama wana-paa wawili,
Ambao ni mapacha ya paa;†
4 Shingo yako ni kama huo mnara wa pembe;
Macho yako kama viziwa vya Heshboni,
Karibu na mlango wa Beth-rabi;
Pua yako ni kama mnara wa Lebanoni,
Unaoelekea Dameski;
5 Kichwa chako juu yako ni kama Karmeli,
Na nywele za kichwa chako kama urujuani,
Mfalme amenaswa na mashungu yake.
6 Jinsi yalivyo mazuri, yalivyo matamu,
Mapenzi katikati ya anasa!
7 Kimo chako kimefanana na mtende,
Na maziwa yako na vichala.
8 Nilisema, Nitapanda huo mtende,
Na kuyashika makuti yake.
Maziwa yako na yawe kama vichala vya mzabibu,
Na harufu ya pumzi yako kama mapera;
9 Na kinywa chako kama divai iliyo bora,
Kwa mpendwa wangu inashuka taratibu,
Ikitiririka midomoni mwao walalao.
10 Mimi ni wake mpendwa wangu,
Na shauku yake ni juu yangu.†

11 Njoo, mpendwa wangu, twende mashambani,
Tufanye maskani katika vijiji.[b]
12 Twende mapema hata mashamba ya mizabibu,
Tuone kama mzabibu umechanua,
Na maua yake yamefunuka;
Kama mikomamanga imetoa maua;
Huko nitakupa pambaja zangu.†
13 Mitunguja hutoa harufu yake;
Juu ya milango yetu yako matunda mazuri,
Mapya na ya kale, ya kila namna,
Niliyokuwekea, mpendwa wangu.†

8 1 Laiti ungekuwa kama ndugu yangu,
Aliyeyanyonya matiti ya mamangu!
Kama ningekukuta huko nje,

Ningekubusu, asinidharau mtu.
[2] Ningekuongoza nyumbani mwa
mamangu,
Naye angenifundisha;
Ningekunywesha divai iliyokolea,
Divai mpya ya mkomamanga
wangu.!

[3] Mkono wake wa kushoto
ungekuwa chini ya kichwa
changu,
Nao wa kuume
ungenikumbatia.!

[4] Nawasihi, enyi binti za
Yerusalemu,
Kwani kuyachochea mapenzi, au
kuyaamsha,
Hata yatakapoona vema?

[5] Ni nani huyu apandaye kutoka
nyikani,
Akimtegemea mpendwa wake?
Nalikuamsha chini ya huo mpera;
Huko mama yako alikuonea
utungu,
Aliona utungu aliyekuzaa.!
[6] Nitie kama muhuri moyoni
mwako,
Kama muhuri juu ya mkono
wako;
Kwa maana upendo una nguvu
kama mauti,
Na wivu ni mkali kama ahera.
Mwako wake ni mwako wa moto,
Na miali yake ni miali ya
Yahu.!
[7] Maji mengi hayawezi kuuzimisha
upendo,
Wala mito haiwezi kuuzamisha;
Kama mtu angetoa badala ya
upendo
Mali yote ya nyumbani mwake,
Angedharauliwa kabisa.!
[8] Tuna umbu mdogo,
Wala hana maziwa;
Tumfanyieje umbu letu,
Siku atakapoposwa?!
[9] Kama akiwa tu ukuta,
Tumjengee buruji za fedha;
Na kama akiwa ni mlango,
Tumhifadhi kwa mbao za
mierezi.!
[10] Mimi nalikuwa ukuta,
Na maziwa yangu kama minara;
Ndipo nikawa machoni pake
Kama mtu aliyeipata amani.!

[11] Sulemani alikuwa na shamba la
mizabibu huko Baal-hamoni
Akawakodisha walinzi hilo
shamba lake la mizabibu;
Kila mtu atoe vipande elfu vya
fedha kwa matunda yake.!
[12] Shamba langu la mizabibu, lililo
langu mimi, li mbele yangu.
Basi, Sulemani, wewe uwe na
elfu zako,
Na hao wayalindao matunda yake
wapewe mia mbili.

[13] Wewe ukaaye bustanini,
Hao rafiki huisikiliza sauti yako;
Unisikizishe mimi.!

[14] Ukimbie, mpendwa wangu,
Nawe uwe kama paa, au ayala,
Juu ya milima ya manukato.!

EGERTON UNIVERSITY LIBRAR